# *Waebrania, Mlango Wa Tano Na Wa Sita* [1]

. . . wa—wa Kitabu cha Waebrania. Ndipo tuingie kwenye wa 7, ukuhani wa Melkizedeki. Na ndipo tuingie, kutoka kwenye ukuhani wa Melkizedeki, tuingie katika siku zile kuu za upatanisho, na kutenganisha, kugawanya vile vipatanisho. Kisha tuingie kwenye ule mlango mkuu wa imani, mlango wa 11. Na mlango wa 12, "Tukiweka kando kila mzigo mzito." Na mlango wa 13, "Yale Makao ya Milele yasiyofanywa kwa mikono ya mwanadamu; bali Mungu, peke yake, ambaye ameyafanya makao haya makuu." Ni ajabu jinsi gani!

2 Nina furaha kumwona dada yetu kule nyuma, ambaye sasa hivi ameingia ibadani. Ninamwona yeye pamoja na mumewe. Jana, tulikuwa tukipanda kwenda zetu, kupitia mahali ambapo . . . Nilifikiri kwamba ninajua kila sehemu yake ndogo, kwa mimi kuwa mlinzi wa wanyama pori hapa Indiana, na nilifanya doria kwa miaka mingi. Nilijua kila sehemu. Lakini ningaliweza kupotea jana, huko juu mahali walikokuwa, juu kwenye zile nundu, barabara mpya.

3 Naye mama huyo alikuwa na kansa kwenye mapafu yake, naye Bwana akamponya kabisa mwanamke huyo. Tulichukua . . . Loo, na jinsi hayo yote yalivyotokea, tulikuwa tumeketi pale. Ndugu Roberson, labda yupo hapa ndani leo. Ninamwona mkewe, pia na Ndugu Woods, ambaye yuko hapa ndani. Nasi tulikuwa tuko juu kule tukiwa kwenye lori la zamani, mimi na Ndugu Roberson, na Ndugu Woods. Basi tulichukua lori hili, tukapanda kwenda kule, juu kwenye kilima. Na huko Bwana akaionyesha ile kansa dhahiri. Na ndipo tukasimama pale na kuiangalia ikimwacha mwanamke huyo. Kwa macho yetu wenyewe, tulisimama na tukaiona ikimwacha mwanamke huyo. Ndipo akampigia simu mke wa Ndugu Wood; naye alikuwa akiniambia, alikuwa akitapika kile kitu cheusi sana. Naye huyu hapa asubuhi ya leo, akiwa ameketi kule nyuma kanisani, yeye na mume wake mpendwa, wakiwa na wakati mzuri sana katika Bwana. Yeye si ni wa ajabu? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

4 Nami sikujua ya kwamba ninii . . . Hapa, kwa kawaida, kwa watu walio karibu, maono yanatokea kwa nadra sana hapa. Hapa ni nyumbani kwangu. Na, ninamaanisha, kanisani.

5 Jumapili, juma moja, sisi . . . Ni wangapi waliokuwa hapa kumwona mtu huyo katika kiti cha magurudumu? Kipofu, mlemavu, hana akili timamu, na neva zake za akilini zimekufa,

nao akina Mayo walikuwa wamemkatia tamaa. Ndipo—ndipo daktari fulani Mkatoliki rafiki yangu alimwambia aje hapa. Na kabla ya kuja ibadani, Bwana alitoa ono la mtu huyo. Ninyi nyote mnajua jambo hilo. Na hapo mtu huyo aliponywa, kwa BWANA ASEMA HIVI. Unaona? Na ndipo akaamka, akatoka kutembea, akachukua kiti chake cha magurudumu, aliweza kuona kama vile ambavyo wewe ungaliweza kuona ama mimi ninavyoweza kuona. Ndipo akatembea akitoka jengoni huku akisukuma kiti chake, yu mzima. Na neva ya akili timamu . . . Unajua, huwezi kusimama. Unaona, ni kwamba tu huwezi. Na kwa miaka mingi imekuwa hivyo.

6 Basi jana nilipofika pale, mama huyo alikuwa anaota ndoto kuhusu kuniona mimi nikiingia, saa nane kamili, na kumtangaza kwamba "ana kansa," na halafu, "BWANA ASEMA HIVI, 'aliponywa.'" Ndipo—ndipo akaamka, na ilikuwa ni saa nane kamili. Ndipo Roho wa Bwana akashuka, na hapo hiyo—hiyo ndoto aliyokuwa nayo, ndipo Bwana akatoa fasiri yake. Naye aliponywa papo hapo, pale pale ambapo tulikuwa tukiangalia. Ni ajabu jinsi gani!

7 Siwezi kukumbuka jina lake. Ni lipi? Jina lako ni nani, dada? Walton, Dada Walton, anayeketi kule nyuma. Waweza kusimama kidogo, Dada Walton? Nataka kukuuliza jinsi unavyojisikia. [Dada Walton anasema, "Vizuri kabisa."—Mh.] Amina. Hilo ni jambo zuri, na safi sana. Yeye ni mwema sana, kutubariki kwa njia hiyo. Kwa hiyo tunatarajia kipimo cha Mungu cha ajabu sana, kikuu mno.

8 Daktari mmoja alikuwa anamficha jambo hili. Alimwambia ya kwamba "alikuwa akipumulia tu kwa upande mmoja." Ilikuwa ni kwamba, kansa ilikuwa imekua toka upande mmoja hadi mwingine na kuziba pumzi ya upande huo wa pafu, unaona. Huwezi kuona kansa kwa eksirei, kwa maana kansa ni seli, yenyewe, na ni—ni uhai. Nawe unaninii . . . Unaninii tu—unaangalia tu kupitia kwenye kansa hiyo, kwa eksirei. Huioni.

9 Na, lakini Bwana kweli ameninii . . . Tulisimama pale na kuiangalia, sisi wenyewe, kwa macho yetu wenyewe. Tukaiona ikisogea, na tukaiona ikitoka, kwa macho yetu wenyewe. Kwa hiyo, tunashukuru sana kwa ajili ya jambo hilo.

10 Na sasa, tuombeeni, juma hili, tunapokuwa tumeondoka. Naye Ndugu Neville labda atachukua toka mahali nilipoachia, kwa ajili ya ibada ya Jumatano usiku. Msiikose sasa, katika mnyororo huu mkubwa wa Kitabu wa Ufunuo.

11 Ninajua maombi mengi yametolewa, nasi tu—tunajua ya kwamba Mungu husikia maombi. Lakini sisi, asubuhi ya leo, tunataka kutoa maombi mafupi tu kabla ya kusomwa kwa Kitabu. Sasa, mtu yeyote anayeweza, anaweza kusoma Kitabu hiki *hivi*, ama anaweza kukifungua namna *hii*. Bali inamhitaji

Mungu, peke yake, kuufungua ufahamu, kwa kuwa Yeye tu Ndiye anayeweza kufanya jambo hilo.

Kwa hiyo na tunaimishe vichwa vyetu kwa muda mfupi.

12 Sasa, Baba, katika Jina la Mwanao mpendwa, Bwana Yesu, tunakuja sasa kwa unyenyekevu sana kujisalimisha wenyewe, kama watumishi Wako, ili upate kunena kupitia kwetu. Itahiri midomo inayonena na maskio yanayosikia, kusudi Neno lipate kunenwa na Mungu na kusikiwa na Roho, ndani ya watu. Tujalie, Baba. Jalia alichukue Neno la Mungu na atuhudumie sisi jinsi tu tulivyo na haja, kwa kuwa tunaomba katika Jina Lake na kwa ajili ya utukufu Wake. Amina.

13 Sasa, usomaji asubuhi ya leo, tunajifunza. Sisi hatuninii—hatuhubiri; tunajifunza tu Kitabu hiki cha Waebrania. Ni wangapi wanaokifurahia? Loo, tunao wakati mzuri sana! Na sasa tunajifunza tu kwa makini, Andiko juu ya Andiko. Hayana budi . . . Biblia nzima, yote inafungamana pamoja. Hakuna hata Neno moja lilillo nje ya mahali pake, kama likiwekwa pamoja na Roho Mtakatifu.

14 Sasa, mwanadamu amesema, "Biblia inajipinga Yenyewe." Ninataka kuona jambo hilo. Nimeuliza, miaka ishirini na mitano, jambo hilo, wala hakuna mtu amepata kunionyesha bado. Biblia haijipingi. Kama inajipinga, si Biblia. Yehova aliye mkuu, asiye na kikomo asingeweza kujipinga Mwenyewe, kwa hiyo hakuna upinzani katika Biblia. Ni kutokufahamu tu kwa watu.

15 Sasa kwa ajili ya msingi mdogo, mpaka tutakaporudi. Sasa, Kitabu cha Waebrania kiliandikwa na Mtakatifu Paulo, kwa Waebrania. Yeye aliandika kimoja kwa Waefeso, hao walikuwa ni watu wa Efeso, Kanisa la Kikristo; kimoja kwa Warumi huko Rumi; na kimoja kwa Wagalatia; na kimoja kwa Waebrania.

16 Sasa, tunaona ya kwamba Paulo, akiwa ni mwalimu wa Biblia, kwanza. Hivyo ndivyo tulivyojifunza. Ya kwamba aliketi chini ya yule mwalimu mkuu, mmoja wa walio wakuu sana wa siku zake, Gamalieli. Naye alitopea sana katika Agano la Kale. Alilijua barabara. Lakini akawa mtesi wa njia iliyokuwa ni Njia ya Kristo, kwa kuwa alikuwa amefunzwa katika Agano la Kale chini ya waalimu. Lakini hao waalimu, wakiwa vile ilivyokuwa ni wa kimwili . . . Ninatumaini sisemi jambo lolote baya.

17 Lakini, kama ilivyo, kama mtu ana fundisho tu na mwelekeo wa shule, kwa kawaida huwa ni kitu kinachobuniwa na binadamu. Unaona, halikuvuviwa, kwa kuwa linakuwa ni fundisho la shule. Tunalo jambo hilo siku hizi. Za Kipresbiteri, za Kilutheri, za Kipentekoste, shule hizi zote zina nadharia zao, nazo zinayapinda tu Maandiko ndani ya shule hizi.

18 Na ilikuwa vivyo hivyo katika Agano la Kale. Lakini, Paulo, akiwa amefunzwa vizuri, na alijua Maandiko kwa neno. Lakini, unaona, Maandiko, haidhuru unayajua vizuri jinsi gani, kama

Roho hayahuishi, basi andiko huua. Roho hutoa Uzima. Unaona, hayana budi kuhuishwa, ama kufanywa hai, na Roho. Roho asipolihuisha Neno na kulifanya halisi kwako, basi andiko hilo ni la kiakili tu. Hapo ndipo tunapokuwa na Wakristo wengi sana wa maneno matupu siku hizi, ama Wakristo wa kujifanya, ni hilo wazo la kisomi la Kristo.

19 Ndipo tulipoinuka kwenye, "Vema, ilibidi ahisi kitu fulani; nawe eti ilikubidi ufanye kitu fulani." Na, loo, tutayaingilia hayo yote, muda si muda. Mtu ilibidi apaaze sauti. Wamethodisti walikuwa lazima mtu apige makelele, kabla hawajampokea. Wapentekoste ilibidi wanene kwa lugha, kabla hawajampokea. Na, loo, baadhi yao, hao Watetemekaji, iliwalazimu kutetemeka. Naam. Wale akina nanii wa kale...Wangetembea huku na huko, wanaume upande mmoja, wanawake upande mwingine. Unaona? Watetemekaji. Ndipo Roho Mtakatifu akawashukia na kuwatikisa. "Walimpokea." Lakini yote ni ndoto za ajabu tu. Hakuna hata mojawapo ya hayo ambayo ni Kweli.

20 Mungu huishi katika Neno Lake. "Imani chanzo chake ni kusikia, kusikia Neno. "Kwa imani mmeokolewa, kwa njia ya neema." Si kwa chochote, ukitetemeka, ama ukinena kwa lugha, ama chochote kinachotukia. Hilo halina uhusiano wowote na jambo hilo, hata kidogo. Yesu alisema, "Yeye ayasikiaye Maneno Yangu na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa Milele. Yeye asikiaye Neno Langu na kuamini, limekwisha kuhuishwa kwake, yuna Uzima wa Milele." Hilo hapo. Haijalishi ni jambo gani dogo unalofanya.

21 Sasa, mimi sipingi kutetemeka, au kunena kwa lugha, wala kutetemeka, loo, huko—huko kupaaza sauti. Hayo ni sawa. Hayo ni mambo mazuri. Ila hizo ni tabia tu. Unaona? Ningeweza kukupa tofaa kutoka kwenye mti, na wewe bado hutakuwa na huo mti. Unaona? Wewe...Ni sifa.

22 Kusema uongo, kuiba, kunywa pombe, kuvuta sigara, kucheza kamari, kuzini, hayo si dhambi, hayo ni matokeo ya kutokuamini. Unaona? Hivyo ndivyo wewe unavyo—unavyoninii...Unafanya hayo kwa maana wewe ni mwenye dhambi. Unaona? Lakini kwanza wewe ni mwenye dhambi. Hilo ndilo linalokufanya ufanye hivyo, kwa sababu huamini. Na kama unaamini, basi hufanyi hayo. Ndipo una upendo, furaha, amani, uvumilivu, wema, utu wema, upole, saburi. Hilo ndilo tunda la Roho Mtakatifu. Unaona?

23 Kwa hiyo tuna mambo madogo-madogo, mihemuko midogo-midogo, ni kwa sababu mwanadamu aliondoka kwenye barabara ya kale iliyotumiwa sana ya Neno. Ni Neno. "Imani chanzo chake ni kusikia."

24 Kwa hiyo wakati Paulo...Mungu alimchagua Paulo. Mwanadamu alimchagua Mathiya. Wakati yeye...Walipiga kura, lakini yeye hakufanya kitu chochote. Hiyo inaonyesha

kanisa lina nguvu za aina gani basi, kujichagulia, kuwachagua mashemasi wao, na kuwatuma wahubiri wao mahali mbali mbali. Hayo ni ya kimwili, mara nyingi.

25 Mwache mtu aende mahali Mungu anakomwongoza kwenda. Ninapenda hilo. Kama watu katika mkutano wanasema tu, "Vema, hili hapa kanisa zuri. Ndugu huyu amejenga kanisa zuri. Nasi tuna maskini mtu mmoja tunayempenda sana." Watamtuma kwenye kanisa hili. Hawatambui ya kwamba wanajiua wenyewe. Unaona? Kwanza, kama mtu huyo akiingia humo, hawezi kupajaza mahali pa mtu huyo. Basi wanalidhoofisha tu kanisa, kujaribu kuonyesha upendeleo kwa mtu fulani wanayempenda. Imekuwa hivyo daima.

26 Lakini ninaamini katika mamlaka ya juu kabisa ya kusanyiko la kitongoji cha mahali fulani hapo. Naam. Acha kila kanisa lijitawale lenyewe, lijichagulie wachungaji wake, mashemasi wake, ninii wake, chochote kile. Na ndipo, kwa njia hiyo, mtu aliyepo hapo hana askofu juu yake. Roho Mtakatifu akitaka kuliambia kanisa hilo jambo fulani, haiwabidi kumwuliza mtu yeyote kuhusu kama wangeweza wafanye *hivi* ama wafanye *vile*. Ni mtu huyo binafsi akiwasiliana na Roho Mtakatifu. Nionyeshe kwa Biblia ni kitu gani kilicho kikuu zaidi, katika Biblia, kuliko mzee wa mahali hapo wa kanisa la kitongoji fulani? Hiyo ni kweli, naam, bwana, mamlaka ya kanisa la mahali pale, kila kanisa lijitegemee lenyewe. Sasa, undugu, huo ni mzuri sana. Makanisa yote yanapaswa kuwa katika undugu kama huo, pamoja. Jambo la pekee ni mamlaka ya juu kabisa ya kanisa la mtaa!

27 Mwangalie Paulo, akiwa ni mwalimu mkuu na hodari, amefunzwa vizuri, akienda zake Dameski, siku moja, kuwakamata watu waliokuwa katika Njia hii mpya. Sasa, yeye alikuwa ni mwaminifu. Mungu hakuhukumu kwa uaminifu wako. Sijapata kuona watu walio waaminifu zaidi kuliko makafiri. Wengi wao hata huwaua watoto wao wenyewe, bure, kwa—kwa kuitolea sanamu dhabihu. Si suala la uaminifu. Mtu angeweza kunywa asidi ya kaboliki, kwa uaminifu, akifikiri alikuwa akinywa kitu kingine. Uaminifu haukuokoi. "Ipo njia inayoonekana kuwa ni sawa kwa mtu, bali mwisho wake ni njia za mauti."

Paulo alikuwa ni mwaminifu wakati aliposhuhudia, katika mamlaka yake mwenyewe, kumpiga Stefano mawe. Miaka mingi baadaye, ninapenda kuomba radhi kwa Paulo, yeye alisema, "Sistahili kuitwa mwanafunzi wala kuitwa mtume, kwa maana nililitesa Kanisa hata kufa." Kwa uaminifu!

28 Na akienda zake, yeye alipata tukio. Roho Mtakatifu alitokea katika Nguzo kubwa ya Moto, nayo ikampofusha. Sasa, tumepitia hayo, hiyo Nguzo ya Moto ilikuwa ni Kristo. Naye ndiye Nguzo ile ile ya Moto iliyowaongoza wale wana kupitia

jangwani. Kristo alikuwa ni Mungu, naye Mungu alikuwa ni Kristo. Mungu alifanyika mwili na akakaa katika mwili wa Bwana Yesu. "Mungu alikuwa ndani ya Kristo, akiupatanisha ulimwengu kwa nafsi Yake," akionyesha kile alichokuwa.

29 Katika Biblia hapa nyuma, katika vifungu vilivyotangulia ambavyo tumekuwa tukisoma, ya kwamba, "Alijifanya Mwenyewe mdogo punde kuliko Malaika. Akachukua umbo, si la Malaika, bali alichukua umbo la mwili." Malaika hawakuwa wameanguka, hawahitaji ukombozi. Mtu alikuwa ameanguka, wanadamu, nao walihitaji ukombozi. Kwa hiyo, katika torati ya kale, mtu, kusudi apate kuwa m—mkombozi, kwanza ilimpasa awe ni ndugu; kile Kitabu kikuu cha Ruthu, tulikipitia hapa, wakati fulani uliopita. Na jinsi ambavyo Mungu, akiwa Roho, alifanyika wa jamaa yetu, kwa kufanyika mmoja wetu, kusudi atukomboe na kutupa Uzima wa Milele. Ilibidi afanyike mmoja wetu, ili kwamba sisi kwa neema tupate kufanyika kama Yeye.

30 Nasi tunaona Nguzo ya Moto iliwaongoza wana wa Israeli. Na wakati ilipofanyika mwili hapa duniani, tunamsikia Yeye akizungumza siku moja, Naye alidai ya kwamba Yeye alikuwa ndiye ile Nguzo ya Moto. Wao walisema, "Unasema ya kwamba wewe ni mkuu kuliko baba yetu Ibrahimu?"

31 Akasema, "Yeye Ibrahimu asijakuwako, MIMI NIKO." MIMI NIKO alikuwa ni nani? Ile Nguzo ya Moto katika kijiti kilichowaka moto, kumbukumbu la milele katika kila kizazi; si kwenye kizazi hicho tu, bali pia na kizazi hiki, Nguzo ile ile ya Moto. Nasi tunashukuru asubuhi ya leo ya kwamba hata tuna picha Yake, ya kwamba Yeye hajabadilika. Yeye ni Yule asiyepatikana na Mauti, wa Milele, Mwenye Kuhimidiwa. Yeye anafanya mambo yale yale wakati huu ambayo aliyafanya nyakati zile, na jinsi hilo linavyotufanya tujisikie wenye furaha.

32 Lakini kabla Paulo hajakubali tukio hili. . .Akijua ya kwamba Malaika wa Bwana alikuwa ndiye ile Nguzo ya Moto, ambayo ilikuwa ni Kristo, ninii. . .Vema, Yeye alikuwa ni yule Malaika wa Agano, ambaye alikuwa ni Kristo. Musa aliwazia ni jambo la thamani zaidi, hivi kwamba, alichagua afadhali ateseke pamoja na watu wa Kristo, na kuongozwa na Kristo, kuliko hazina zote za Misri. Yeye alimfuata Kristo, ambaye alikuwa katika umbo la Nguzo ya Moto.

33 Ndipo Kristo akasema, "Nilitoka kwa Mungu," wakati alipokuwa hapa duniani, "Ninarudi kwa Mungu." Baada ya mauti Yake, kuzikwa, kufufuka, mwili uliotukuzwa ukiketi mkono wa kuume wa Ukuu, kufanya upatanisho; Paulo alimwona kama Nguzo ya Moto, tena: Nuru ambayo karibu impofushe macho; ilimpiga upofu.

34 Petro alimwona akiingia gerezani kama Nuru, na kuifungua milango mbele zake alipokuwa akitoka. Tunaona ya kwamba Yeye alikuwa ni Alfa na Omega, wa Kwanza na wa Mwisho.

35 Naye huyu hapa pamoja nasi, leo, akifanya mambo yale yale aliyofanya wakati ule, akijifanya Mwenyewe aonekane kwetu tena, akiuonyesha ulimwengu wa kisayansi jambo hilo.

36 Loo, katika saa hii kuu ya giza na machafuko juu ya nchi, tunapaswa kuwa watu walio na furaha sana duniani kote, kufurahi, kwa kujua. Wakati wote, wakati watu wameshindiliwa kasumba, na kila aina za itikadi na mambo chungu mbovu yaliyoko duniani, na hata hivyo, leo, yule Mungu halisi, aliye hai, kwa Neno Lake na kwa thibitisho Lake linaloonekana, anatuonyesha ya kwamba Yeye yuko hapa pamoja nasi, akitenda kazi, akitembea, akiishi, akifanya vile vile kabisa kama alivyofanya daima. Sisi ni watu waliopendwa jinsi gani, kupata jambo hili! Inatupasa kuninii . . . Biblia ilisema, basi, katika mlango wa pili, "Inatupasa kushikilia sana mambo haya. Kwa sababu, na sisi je! tutapataje kupona kama tusipoujali wokovu mkuu namna hii?"

37 Sasa, tumekuja kuona, kabla Paulo hajakubali tukio hilo . . . Sasa, tunachimbua. Sasa, haidhuru ni tukio la jinsi gani utakalopata kuwa nalo, enyi kanisa, ninataka kuwauliza jambo fulani. Haidhuru litaonekana ni zuri jinsi gani, jinsi linavyoonekana kuwa ni halisi, halina budi kwanza kujaribiwa kwa Biblia. Daima kwenye Neno! Kamwe usiliache Hilo, kwa tukio la aina yoyote.

38 Naye Paulo, kabla hajalikubali hilo, alishuka akaenda huko Arabuni, na huko alikaa miaka mitatu, akichunguza tukio hili kwa Neno. Na aliporudi, alikuwa na hakika. Hakuna kitu kingaliweza kumbadilisha, kwa kuwa alikuwa amesimama imara kabisa juu ya Neno, bila kutikiswa. Na hapa sasa ndipo anapogeuka kuwaonyesha hawa Waebrania, mambo hayo makuu yaliyonenwa, ya Agano la Kale, yalidhihirishwa katika Yesu Kristo. Ni utukufu wa jinsi gani!

39 Sasa, Jumapili iliyopita, ama Jumatano iliyopita, Ndugu Neville hapa, katika mlango wa 5, aligusia baadhi ya sehemu muhimu sana, kwa kuwa ni mlango mzuri sana. Nasi tunamwona akishughulika kwenye mlango wa 4, Jumapili iliyopita, juu ya *Sabato*, kuadhimisha Sabato. Mna hakika, asubuhi ya leo, mnajua kuadhimisha Sabato ni kitu gani? Kama mnajua, semeni, "Amina." [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

40 Sabato ni "Raha" tunayoingia, si kwa siku, si kwa torati, bali ni kwa kuingia ndani ya Kristo ambaye ndiye Sabato yetu. Yeye Ndiye Sabato yetu. Tuliyapitia hayo yote katika Agano la Kale, na kuonyesha ya kwamba wakati ungekuja ambapo Neno lingekuja "kanuni juu ya kanuni, amri juu ya amri." Naye alithibitisha ya kwamba tuliingia katika Raha Yake kwenye Siku ya Pentekoste, "Kwa kuwa hii ingempa raha aliyechoka, kukoma."

41 Tunaona, ya kwamba, "Mungu aliweka siku katika Daudi, kuhusu siku ya saba." Na, "Mungu alistarehe kwenye ya saba." Akaitoa kwa—wana wa Israeli huko jangwani. "Na tena, yeye aliweka siku." Ilikuwa ni siku gani? Siku fulani ya juma? "Siku utakapoisikia Sauti Yake, usiufanye mgumu moyo wako." Hiyo ndiyo siku anayoingia, apate kukupa wewe amani ya Milele, Sabato ya Milele.

42 Huendi kanisani Jumapili, upate kuwa wa kidini, basi. Unapozaliwa na Roho ya Mungu, unaingia katika Raha milele, hakuna tena kuadhimisha sabato. Uko *katika* Sabato, sikuzote, daima, na kwa Umilele. "Kazi zako za kilimwengu zimekwisha," yasema Biblia, "nawe umeingia katika amani hii iliyobarikiwa."

43 Milango hii mitano ya kwanza inamweka Yesu mahali pake kama Kuhani Mkuu. "Mungu alisema zamani na baba zetu katika manabii kwa sehemu nyingi na kwa njia nyingi, lakini katika siku hii ya mwisho kwa Mwanawe, Yesu," mlango wa 1, kifungu cha 1.

44 Halafu moja kwa moja chini kufikia mwisho wa mlango wa 5, tunamwona amewakilishwa kama "Melkizedeki, ambaye hakuwa na mwanzo wa siku Zake, wala mwisho wa uhai wake, bali anadumu Kuhani milele." Wazia jambo hilo. Je! Mtu huyu mkuu alikuwa ni nani? Tutalipata hilo, katika kama milango mingine miwili zaidi. Maisha Yake yote, tutayasoma. "Mtu Huyu mkuu aliyekutana na Ibrahimu, ambaye kamwe hakuwa na baba yeyote, hakuwa kamwe na mama yeyote. Hakuwa na wakati wowote aliopata kuanza maisha, wala kamwe hatakuwa na wakati ambapo maisha Yake yatakoma. Naye alikutana na Ibrahimu akitoka katika kumpiga mfalme."

45 Mwangalie Mtu huyu mkuu, yeyote aliyekuwa, angali yu hai. Hakuwa na mwisho wa uhai Wake. Ilikuwa ni Kristo, aliyekutana naye. Tunaingia kwenye somo lenye kilindi juu ya jambo hilo, katika siku chache.

46 Sasa, tunataka kuanzia hapa kwenye mlango wa 5 sasa, kwa ajili ya msingi mdogo tu kabla hatujafikia wa—wa 6, kwa kuwa kwa kweli ni kitu cha ajabu sana. Angalieni kwa makini. Tutaanzia karibu kwenye kifungu cha 7 cha mlango huu. Vema, hebu na tuanzie kwenye kifungu cha 6.

> *Kama asemavyo mahali pengine, Ndiwe kuhani milele kwa mfano wa Melkizedeki.*
>
> *Yeye, siku zake hizo za mwili wake, alipomtolea yule, awezaye kumwokoa na kumtoa katika mauti, maombi na dua pamoja na kulia sana na machozi, akasikilizwa kwa jinsi alivyokuwa mcha Mungu;*
>
> *Na ingawa* alikuwa *ni Mwana, alijifunza kutii kwa mateso hayo yaliyompata,*

47 Sasa hapa ndipo ninapotaka kufikia, hiki kifungu cha 9. Sikilizeni. Ninadhani Ndugu Neville alipagusia, Jumatano. Sikuwa hapa. Vema, sikilizeni.

*Naye alipokwisha kukamilishwa, akawa sababu ya wokovu wa milele kwa watu wote wanaomtii;*

*Kisha ametajwa na Mungu kuwa kuhani mkuu kwa mfano wa Melkizedeki.*

*Ambaye tuna maneno mengi ya kunena habari zake, . . .*

48 Tutayaachia hapo kwenye jambo hilo, maana tutamchukua Melkizedeki katika siku chache zijazo usiku.

49 Sasa tutaanza kwenye hili, somo letu la kawaida. Laiti . . . Nitasoma tu haya mengine kwa muda mfupi, kifungu cha 11

*Ambaye tuna maneno mengi ya kunena habari zake; . . . na ni shida kuyaeleza kwa kuwa mmekuwa wavivu wa kusikia.*

*Kwa maana, iwapasapo kuwa waalimu, (maana wakati mwingi umepita), mnahitaji kufundishwa na mtu mafundisho ya kwanza ya maneno ya Mungu; nanyi mmekuwa mmehitaji maziwa wala si chakula kigumu.*

*Kwa maana kila mtu atumiaye maziwa hajui sana neno la haki, kwa kuwa ni mtoto mchanga.*

Loo, ninatumaini ya kwamba Roho Mtakatifu amelichukua hilo akaliingiza moja kwa moja ndani yenu sasa.

*Kwa maana kila mtu a—atumiaye maziwa hajui sana neno la haki; kwa kuwa ni mtoto mchanga.*

50 Ukimpa mtoto chakula kigumu, utamwua. Hiyo ndiyo sababu watu wengi sana husema, “Aa, si—siamini jambo hilo,” na kuondoka kwenda zao. Wangali ni watoto wachanga! Kamwe hawawezi kabisa kufahamu. Kamwe hawawezi kuelewa na Kweli hiyo. Ina—Inawaua. Mambo makubwa yenye nguvu ambayo kanisa linapaswa kuyajua leo, bali usingeweza kulifundisha. Wa—wa—wa—wa—wanajikwaa kwenye Hilo. Hawajui wafanye nini Nalo.

51 Paulo, akinena na kundi hili la Waebrania . . . Hata hivyo, anawazungumzia wasomi sasa, wasomi, waliobobea. Tunaona hilo, katika muda m—mfupi, ni wasomi sana. Lakini Siri kuu ya kiroho, kanisa lingali ni kipofu Kwake. Yeye alisema, “Wakati inawapasa kuwa mkiwafundisha wengine, wewe ungali u mtoto mchanga.”

52 Loo, ninajua kuna wengi wanasimama na wanatoka na kwenda kusema, “Loo, sihitaji kwenda kanisani tena. Mungu asifiwe, Roho Mtakatifu amekuja, Yeye ndiye mwalimu.” Unapopata wazo hilo, umekosea tu. Kwa kuwa ni kwa nini Roho Mtakatifu aliwaweka waalimu kanisani, kama Yeye atakuwa

mwalimu? Unaona? Kwanza kuna mitume, manabii, waalimu, wainjilisti, na wachungaji. Roho Mtakatifu aliweka waalimu kanisani, ili aweze kufundisha kupitia kwa mwalimu huyo. Na kama si—si kulingana na Neno, Mungu halithibitishi, basi si fundisho lililo sahihi. Halina budi kulingana na Biblia nzima, na liwe hai tu siku hizi kama lilivyokuwa wakati huo. Hilo hapo jambo halisi lililothibitishwa.

53 Sasa angalia.

> *Lakini chakula kigumu ni cha watu wazima, ambao akili zao, kwa kutumiwa, zimezoezwa kupambanua mema na mabaya.*

Kujua mema na mabaya, kwa upambanuzi.

54 Sasa angalia, tukianza sasa juu ya somo letu. Huu msingi mkubwa sasa, hebu na tukiendee kifungu cha kwanza.

> *Kwa sababu hiyo, tukiacha kuyanena mafundisho ya kwanza ya Kristo, . . .*

Ati anasema nini? Milango hii yote mitano ya kwanza imewekwa juu ya Kristo, kuonyesha kwamba Yeye ni nani. Sasa tunaacha hayo mafundisho ya kwanza ya Kristo.

55 Tunamwona kwamba Yeye ni nani? Tulimwona kuwa ni Yehova Mungu aliye Mkuu aliyedhihirishwa katika mwili. Tulimwona a—akiwa si nabii, bali ni utimilifu wa Mungu kwa jinsi ya mwili. Yeye alikuwa ni Yehova aliyefanyika mwili. Nao mwili huo, Yesu, ulimfanyia tu maskani. Mungu akiishi katika mwanadamu. Mungu akipatanishwa na mwanadamu, kupitia kwa mwanadamu, kwa kuzaliwa kibikira kwa Mwanawe Mwenyewe. Naye Yehova, yule Roho, alikaa ndani Yake.

56 Sasa, ni wangapi wanakumbuka mafundisho juu ya Uungu, jinsi tulivyorudi nyuma tukampata Mungu kama vile upinde mkuu wa mvua akiwa na Roho hizo zote mbalimbali, jinsi ilivyokuwa? Ndipo Logos akatoka kwa Mungu, ambaye alifanyika thiofani, nayo ilikuwa katika umbo la mwanadamu. Naye Musa alimwona akipita, akiwa kwenye ufa wa mwamba. Ndipo huyo thiofani baadaye ilifanyika mwili wa mwanadamu kabisa, Kristo.

Na jinsi tunavyoona ya kwamba sisi, kwa neema Yake, tuna Uzima wa Milele. Sasa, neno *daima* ni "kwa umbali fulani; kwa kipindi fulani cha wakati." Ilinenwa, katika Biblia, "Milele *na* milele," kiunganisho. Lakini *daima* linamaanisha tu "wakati fulani." Lakini Milele linamaanisha bila kikomo. Na ni kila kitu tu kilichokuwa na mwanzo ndicho kilicho na mwisho, bali vitu visivyokuwa na mwanzo havina mwisho. Kwa hiyo Mungu hakuwa na mwanzo wala hana mwisho.

57 Na kwa hiyo, basi, Melkizedeki, yule Kuhani mkuu, kama mwanadamu, Yeye hakuwa na mwanzo wala hana mwisho. Na wakati sisi, kupitia thiofani hiyo, ambapo, tulifanywa katika

sura ya Mungu kabla ulimwengu haujapata kuumbwa; wakati hiyo thiofani imefanyika mwili na kukaa kwetu, basi, kwa mauti Yake, sisi wenyewe tunapokea Roho Wake na hatuna mwisho; Uzima wa Milele; si Malaika, bali ni wanaume na wanawake. Loo, mimi . . . Kwa namna fulani, laiti ningaliweza kulielezea kwa njia ambayo wasikilizaji wa—wangu wangeweza kulipata! Kamwe hutakuwa Malaika. Mungu aliumba Malaika, bali Mungu alimwumba mwanadamu. Na yale Mungu aumbayo yanatokana na Mungu, ambayo ni ya Milele kama Mungu alivyo wa Milele. Na mwanadamu ni wa Milele tu kama vile Mwumba wake, kwa maana aliumbwa kutoka Umilele.

58 Lakini dhambi ina mwisho, mateso yana mwisho. Kwa hiyo, hakuwezi kuwepo na jehanamu ya Milele. Kuna jehanamu, moto na kiberiti, tunajua jambo hilo, lakini hakuna jehanamu ya Milele. Kuna aina moja tu ya Uzima wa Milele na huo ni wa Mungu. Kama utateseka milele, una Uzima wa Milele. Jahanamu ina mwisho, huenda ikawa ni mabilioni ya miaka, bali hatimaye itakwisha.

59 Biblia haisemi, mahali popote, ya kwamba waliteseka Milele, ilisema, "Daima na daima." Yona alifikiri alikuwa katika tumbo la nyangumi "sikuzote," pia. *Sikuzote* ina umbali ama kipimo cha wakati. Bali *Milele* ni pasipo mwisho, haina mwanzo wala mwisho. Ni kama pete, duara. Na wakati muda wetu unapoendelea, tunazunguka-zunguka tu kwenye nia kuu za Mungu.

60 Kusudi la Mungu lilikuwa ni kumfanya mtu katika mfano Wake, apate kufanya ushirika pamoja Naye. Naye alimfanya anayeweza kuwa kiumbe kinachoweza kushikika. Sasa, dhambi ilituleta mahali pa—pa—pa upotovu, bali hilo kamwe halikomeshi mpango wa Mungu. Na, ewe rafiki mwenye dhambi, leo, kama hujazaliwa mara ya pili kwa Roho wa Mungu, una mwisho mahali fulani. Na mwisho wako ni machafuko, katika maangamizi, na mateso, na maumivu. Lakini kwenu ninyi mliomwamini Bwana Yesu, na kumkubali vivyo hivyo kama Mwokozi wenu binafsi, ninyi ni jambo la Milele tu kama Mungu alivyo wa Milele. Hamna mwisho, "Ninawapa Uzima wa Milele wa *Zoe*, Uzima wa Mungu Mwenyewe, wala hawataangamia wala kuja hukumuni, bali wamepita toka mautini kuingia Uzimani." Hivyo ndivyo Yeye alivyokuwa. Hicho ndicho alichojia.

61 Sasa, Yesu, katika kuja Kwake, kwa ukuhani Wake, hakuja eti kusudi ahurumiwe. Watu wengi hufundisha jambo hilo hivyo, ya kwamba Yeye alikuja, akisema, "Vema, labda kama nikiteseka, nitakuwa ki—ki—kitu cha kuhuzunisha na ndipo watu hakika watanijia Mimi." Hilo ni kosa. Hakuna Andiko kwa jambo hilo.

Kwa kuwa, kila mtu atakayepata kuokolewa, Mungu aliwajua kabla hata ya kuumbwa kwa ulimwengu. Biblia ilisema hivyo. "Mungu hapendi sasa mtu yeyote apotee." Anataka wote waifikie toba. Lakini, akiwa ni Mungu, kwa kutangulia kujua tangu zamani Yeye alijua jambo hilo.

62 Angalia katika Warumi, mlango wa 8. Paulo alikuwa akishikilia pale juu, akisema kuhusu uteuzi wa Mungu, ya kwamba, "Esau na Yakobo, kabla ya mmojawapo wa hao watoto wachanga kuzaliwa, ama chochote kile, Mungu alisema ya kwamba aliwajua na alimchukia Esau na kumpenda Yakobo," kabla mmojawapo wa wavulana hao haja—hajapata nafasi ya kutoa shukrani zao, kwa kuwa Yeye alikuwa ni Mungu. Yeye anajua . . . Yeye hana kikomo. Kama Yeye hana kikomo, Yeye alijua kila kiroboto, kila nzi, kila usubi, kila kitu ambacho kitakuwako duniani. Yeye alikijua. Yeye ni Mungu asiye na kikomo, wa Milele, asiyepatikana na mauti, aliyetukuka, mwenye nguvu zote, aliyepo mahali pote, ajuaye yote. Hakuna kitu asichojua. Hiyo ndiyo sababu Yeye anaweza kujua mwisho utakuwa nini. Alijua mwisho tangu mwanzo.

63 Kilicho cha kinabii ni ujuzi Wake tu. Yeye ndiye hakimu mkuu. Yeye, Yeye ni ninii . . . Yeye ni hakimu. Naye anamwambia tu mwana—mwanasheria kiasi tu cha hekima Yake. Na hivyo ndivyo unabii ulivyo, ambao anaweza kutabiri, kwa kuwa Yeye anajua kitakachokuwako. Sasa, huyo hapo huyo Mungu tunayemtumikia. Si mungu fulani wa historia, si kama akina Budha, na akina Mohamedi, na kadhalika. Bali, Mungu ambaye yupo mahali pote, papa hapa sasa, asubuhi ya leo, katika maskani hii sasa hivi; Yehova Mkuu, MIMI NIKO, Ambaye alijiumba katika unyenyekevu, apate kuchukua mfano wa mwili wenye dhambi. Yuko hapa. Huyo ndiye aliyekukomboa. Hakuwezi kuwako na mwingine, popote, wakati wowote anayeweza kufanya jambo hilo.

64 Mungu hakuwa na watu watatu huko juu, Naye akamtuma mmoja wao, Mwanawe. Ilikuwa ni Mungu, Mwenyewe, aliyeshuka katika mfano wa Mwana. Mwana yeyote ana mwanzo, na huyo Mwana alikuwa na mwanzo. Huyo, baadhi yenu ninyi Wakatoliki wapendwa, nina kitabu chenu, *Ukweli wa Imani Yetu*, kilisema, "Umilele wa uwana wa Mungu." Utalielezeaje neno hilo? Utalifanyaje lieleweke? Lawezaje hilo kuwa ni la Milele? Hiyo si Biblia. Hicho ni Kitabu chenu, "Uwana wa Milele." Hawaninii . . . Neno hilo si sahihi. Kwa kuwa, chochote ambacho ni mwana kilikuwa na mwanzo, na Milele haina mwanzo, kwa hiyo si uwana wa Milele. Kristo alifanyika mwili na akakaa kwetu. Yeye alikuwa na mwanzo. Hakukuwako na uwana wa Milele. Ni Uungu wa Milele, si uwana. Sasa, Yeye alikuja kutukomboa, Naye alitukomboa.

65 Sasa, Paulo, akifikia pale, jambo ambalo nina hakika ya kwamba kupitia kwenye masomo yaliyopita mmelifahamu.

Tutalirudia tena, wakati mmoja, Bwana akipenda, kifungu tu kwa kifungu, sasa.

> *Kwa sababu hiyo, tukiwa . . . tukiacha kuyanena ma— mafundisho ya kwanza ya Kristo, tukaze mwendo ili tuufikilie utimilifu; . . .*

66 Hilo huwakwaza. Sivyo? Ati na tufanye nini?

> *. . . na tukaze mwendo ili tuufikilie utimilifu; tusiweke tena* misingi . . .

67 Angalia jambo hili. Hebu na tuchukue neno hili "utimilifu." Je! Unajua kuna njia moja tu utakayosimama kwayo Mbele za Mungu? Hiyo ni, kutimilika. Mungu hawezi kuvumilia vitu vichafu.

68 Na ninyi washika sheria: mngewezaje kujikamilisha, wakati hamna hata jambo moja la kujikamilisha nalo? Mlizaliwa katika dhambi. Kuchukuliwa mimba kwenu kwenyewe kulikuwa katika dhambi. Tamaa yenu yenyewe ya kuwa hapa ilikuwa ni dhambi. "Mlizaliwa katika dhambi, mkaumbwa katika uovu, mkaja ulimwenguni mkisema uongo." Sasa mtasimama wapi?

69 Uko wapi, ewe mwenye dhambi, u—uliyesema, "Nitaacha kuvuta sigara. Nitaenda Mbinguni"? Uko wapi, ewe unayejiita Mkristo, vuguvugu, uliyejaa kuvumwani, unayetembea hapa umekunja uso na kusema, ya kwamba, "Vema, mimi ni mfuasi wa kanisa"? Ewe mwenye dhambi. Hiyo ni kweli. Isipokuwa umezaliwa kwa Roho wa Mungu, umepotea. Hiyo ni kweli.

70 Utaendaje Mbinguni? Unasema, "Sijapata kusema uongo maishani mwangu. Loo, maskini kipenzi hicho. Ki—kilikuwa tu ni Malaika, kwanza." Huo ni uongo. Sijali wewe ni mzuri jinsi gani; wewe ni mwenye dhambi. Nawe huna hata jambo moja; hakuna kasisi, hakuna askofu, hakuna kadinali, hakuna papa, wala chochote kile kinachoweza kukuokoa, kwa sababu yeye yuko kwenye hali ile ile uliyo nayo. Tutafikia hilo mnamo dakika chache. Yuko kwenye hali ile ile tu uliyokuwa. Papa wa Roma alizaliwa katika dhambi, akaumbwa katika uovu, akaja ulimwenguni akisema uongo, alizaliwa kwa tamaa ya kujuana kimwili ya mwanamume na mwanamke. Utapata wapi utakatifu kutoka katika jambo hilo?

71 "Vema, baba yake na mama yake walizaliwa kwa njia ile ile, nao walizaliwa kwa njia ile ile, na bibi yake na babu yake na moja kwa moja kurudi huko nyuma." Ni dhambi, kwanza!

72 Kwa hiyo ni nani anayeweza kusema ya kwamba *huyu* ni mtakatifu na *yule* ni mtakatifu? Kuna kitu kimoja tu kilicho kitakatifu, hicho ni Yesu Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai, Ambaye amefanywa Mtimilifu. Nasi hitaji letu ni kuwa watimilifu. Sasa, tutakuwaje hivyo? Hebu jaribu hilo, wewe mwenyewe. Nisingetaka kujaribu kwenda Mbinguni kwa stahili ya, "Nilizaliwa dakika tano zilizopita, na ninaondoka

ulimwenguni sasa hivi." Ningepotea. Nisingalikuwa kamwe na wazo baya maishani mwangu, nisingalisema neno baya maishani mwangu, kama nisingaliangalia kitu chochote kibaya, sikuwazia kamwe jambo lolote baya, wala chochote kile, ningali nimeoza na ni mweusi kama kuta chafu sana za kuzimu. Mimi ni mwenye dhambi.

73 Ningeweza kupitia maishani na nifungiwe chumbani, na kama baadhi ya masista wa Karmeni ama chochote kile, wala nisiuone ulimwengu, nikae mle ndani na kuomba maishani mwangu mwote, nitende mema, nizaliwe tajiri nikiwa milionea sana na niwape maskini kila kitu nilicho nacho, na ningali ni mwenye dhambi na nitaenda jehanamu. Naam, bwana.

74 Ningeweza nikajiunga na kanisa la Kilutheri, Kibaptisti, Kipentekoste, Kipresbiteri, tangu nikiwa kwenye kitanda kidogo cha mtoto, na niishi mwaminifu kwa kanisa hilo mpaka nifikie miaka mia moja, na uhai wangu uondolewe, wala hakuna mtu angeweza kunielekezea kidole na kusema "Kamwe hajapata kuwa na hata wazo moja baya," nitaenda jehanamu kwa hakika tu kama ninavyosimama.

75 Mimi ni mwenye dhambi. Hilo ni kweli. Sina kitu. Hakuna njia, hata kidogo, ningeweza kupata gharama yo—yoyote ya kulipiwa. Mungu alihitaji kifo. Na kama nikiyatoa maisha yangu mwenyewe, kama nikiyatoa maisha yangu, basi ninawezaje kutubu? Maana, wewe. . .Deni halina budi kulipwa, kwanza. Na Mungu alikuwa Ndiye pekee angaliweza kuutoa uhai Wake na kuutwaa tena. Kwa hiyo angeweza kufanyika dhambi, na kuweka Uhai Wake chini na kuutwaa tena, na kuita jambo hilo "haki," na deni imelipwa. Haya basi.

76 Sasa hebu na tufungue katika Mathayo, kwenye mlango wa 8, ninaamini ndipo, mlango wa 7 ama wa 8. Tutaona yale Yesu anayosema hapa. Vema. Ni Mathayo, mlango wa 5. Na ninii. . . Yesu, kuhubiri, akihubiri katika zile heri, kifungu cha 47.

> *Tena mkiwaamkia ndugu zenu tu, mnatenda tendo gani la ziada? Hata watu wa mataifa, je!. . .?* (Angalia?)
>
> *Bali ninyi mtakuwa wakamilifu,* (Ati nini?)
>
> *Basi ninyi mtakuwa wakamilifu, kama Baba yenu wa mbinguni alivyo mkamilifu.*

Hiyo ilikuwa ni amri ya Yesu, "Mwe hivyo."

77 Wao wanasema, "Hakuna mtu anayeweza kuwa mkamilifu, Biblia ilisema, 'Hakuna mtu mkamilifu.' Huko hapo kuhitilafiana kwako." Sivyo? Vema.

78 Huwezi kuwa mkamilifu kwa nafsi yako. Kama unatumainia yale uliyofanya, umepotea. "Kwa hiyo iweni wakamilifu, wakamilifu tu kama vile Mungu alivyo mkamilifu." Sasa:

> *Basi ninyi mtakuwa wakamilifu, kama Baba yenu. . . mbinguni alivyo mkamilifu.*

79 "Kwa sababu hiyo..." Sasa, mlango wa 5, mlango wa 6 wa Waebrania.

> *Kwa sababu hiyo, tukiacha kuyanena mafundisho ya kwanza ya Kristo, tukaze mwendo ili tuufikilie utimilifu;...*

80 Sasa, ninyi, Maskani ya Branham. Loo, ninajua, "Tuna uponyaji." Hilo ni jambo zuri sana. "Tuna maono." Loo, hilo—hilo ni sawa. Na mna ndoto za kiroho, na wakati mwingine si za kiroho. Na—na wakati mwingine mnaninii... "Sisi, sisi tunajaribu kuwasaidia maskini. Tunafanya tuwezayo." Loo, hayo ni sawa, bali hayo siyo tunayozungumzia sasa. Tunaingia kwenye kipindi kingine.

> *...tukiacha...mafundisho...*

81 "Loo, ndio, tuna fundisho la Kristo. Tunaamini alikuwa ni Mwana wa Mungu, alizaliwa na bikira. Tunaamini hilo, pamoja na mambo haya yote." Hilo ni zuri tu.

82 Lakini, "Tukiacha hayo, na tukaze mwendo ili tuufikilie utimilifu." Loo, jamani! Laiti ningalikuwa na sauti ya malaika mkuu sasa, kuleta jambo hilo mahali ambapo mngeweza kuliona. Sasa yeye anasema, "Tukiacha kuyanena mafundisho yote ya Kristo," wa—wanatheolojia wote, na theolojia yote tunayojua, yote yanayohusiana na Uungu wa Kristo, jinsi alivyokuwa ni Mungu aliyefanyika mwili, mambo haya mengine yote.

83 Paulo anaendelea kuyaelezea yote hapa, katika dakika chache tu. Hebu na tuyasome tu, kidogo tu, kabla hatujalifikia.

> *...tusiweke* misingi *tena wa kuzitubia kazi zisizo na uhai,...*

Sasa, tunaamini jambo hilo.

> *...na wa kuwa na imani kwa Mungu,*

Tunaamini hilo.

> *Na wa mafundisho ya mabatizo,...*

Vile tu unapaswa kubatizwa, tunaamini jambo hilo.

> *...na kuwekea mikono,*

Tunaamini katika kuwekea mikono. Sivyo? Unaona, yote hayo, hakika.

> *...na kufufuliwa wafu,...*

84 Tunaamini hayo. Sasa angalia. Unaona hapa, "Hukumu," linatumiwa, "Milele." Hiyo ni daima. Wakati hukumu ya Mungu inaponenwa, ni ya daima. Basi, haiwezekani kuwako tena na upatanisho baada ya hukumu kukatwa. Sasa mnaweza kufahamu ni kwa nini ilimbidi Mungu kuchukua ninii Yake Mwenyewe—ninii Yake Mwenyewe, kama tunavyosema, dawa Yake Mwenyewe. Wakati alipomhukumu mwanadamu kwa

ajili ya kutenda dhambi, njia pekee ambayo Yeye angeweza kupatanisha, ilikuwa ni Yeye Mwenyewe kupachukua mahali pa mwanadamu. Hivyo ndivyo tu anavyoweza kupatanishwa, ama angeweza kutupatanisha, ilikuwa ni kupachukua mahali petu na afanyike mwenye dhambi. Mungu, Yehova, alifanyika mwenye dhambi, Naye aliutoa uhai Wake.

85 Sasa, ungeweza kuyatoa maisha yako, kama mwenye dhambi, kufa kwa ajili ya jambo fulani. Paulo alisema, "Nijapotoa mwili wangu niungue moto kama dhabihu, ningali si kitu mimi," maana haitafaa kitu. Unaona, unapokufa, umekwisha. Ukifa kama mwenye dhambi, umepotea.

86 "Lakini Mungu alishuka katika mwili, na akaihukumu dhambi katika mwili, akifanyika mwili wenye dhambi." Kwa sababu, Yeye alikuwa ni yule Mungu wa Milele, na akaufufua mwili Wake Mwenyewe, kwa hiyo Yeye ndiye mwenye kuhesabia haki.

87 Sasa, mambo haya yote, "Na tukaze mwendo ili tuufikilie utimilifu," Paulo alisema. Sasa ni nini?

> . . .*na hukumu ya milele.*
>
> . . .*hayo yote* tutayafanya *Mungu akitujalia.* (Kifungu cha 3.)

88 Sasa, "Tukaze mwendo ili tuufikilie utimilifu." Yesu alisema, "Basi ninyi iweni wakamilifu, kama Baba yenu wa Mbinguni alivyo mkamilifu."

Na sisi, kila mmoja wetu, amehukumiwa. Haidhuru tuliwahi kufanya nini, tumehukumiwa. Tulizaliwa, tumekwisha kuhukumiwa. Mama yako na baba walizaliwa, wamekwisha kuhukumiwa. Ninyi, wahenga wenu wote, walizaliwa katika dhambi, wakazaliwa katika uovu. Kwa hiyo utaupataje? Utakuwaje mkamilifu? Kama hujawahi kutenda jambo hata moja, hujaiba, hujasema uongo, hujatenda jambo lolote maishani mwako, ungali umehukumiwa. Ulihukumiwa kabla hujapumua pumzi yako ya kwanza. Ulihukumiwa. Hiyo ni kweli. Na ulihukumiwa na Mungu kabla hujapumua pumzi yako ya kwanza. Kwa kuwa ulihukumiwa, kwa tamaa ya kimwili ya baba yako na mama ambao, kwa tendo lao, walikuleta hapa duniani. Naye Mungu alilihukumu, hapo mwanzo. Kwanza umehukumiwa, tayari. Kwa hiyo wapi wewe. . .Na kila mtu mwingine yeyote duniani alihukumiwa pamoja na wewe. Sasa utapata wapi ukamilifu?

89 Angalia. Hebu na tufungue kwa muda mfupi tu katika Waebrania, mlango wa 10. Sikilizeni kwa makini. Ninataka kusoma kidogo kutoka kwenye mlango wa 9, kwanza, kifungu cha 11.

> *Lakini Kristo akiisha kuja, aliye kuhani mkuu wa mambo mema yatakayokuwapo, kwa hema iliyo*

*kubwa na kamilifu zaidi,* hema *yake* mwenyewe, mwili wake . . .

90 Unaona, lile hema la kale, unaona, lile hema la kale lilikuwa na pazia ndani yake, lililoficha sanduku la agano ambamo Mungu aliishi. Ni wangapi wanaojua jambo hilo? Hakika. Vema, hiyo maskani ya kale iliyotengenezwa na binadamu hapa, pazia zilizotoka kwenye ngozi za mbuzi zilizotiwa rangi, na kadhalika, zilifanywa hema ya kuficha Uwepo wa Mungu. Ni wangapi wanaojua ya kwamba mtu mmoja peke yake ndiye angaliweza kuingia mle mara moja kwa mwaka? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Hakika. Huyo alikuwa ni Haruni, kuingia mara moja kwa mwaka. Naye hana budi kutiwa mafuta. Na—na, loo, masharti! Naye lazima awe ana moto mkononi mwake; na kama aliingia bila ya huo, alikufa mara alipoifungua hiyo pazia. Angeanguka afe. Sharti aingie mle ndani na kuwasha vinara hivi vya taa, na anyunyizie kiti cha rehema kilichowakilisha, damu ya mauti, ya kibadala, mpaka Kristo alipokuja kuyatimiza hayo.

91 Sasa, lakini, Mungu basi alifanyika maskani ya aina nyingine. Na maskani hiyo ilikuwa ni nani? Yesu. Naye Mungu alikuwa ndani ya Yesu, Naye alikuwa amefichwa, bali alikuwa akiupatanisha ulimwengu kwa nafsi Yake, kwa madhihirisho Yake. Kristo alimfunua Mungu. Yeye alisema, "Si Mimi nifanyaye kazi hizi. Ni Baba Yangu anayekaa ndani Yangu. Sifanyi neno Mimi Mwenyewe ila yale nimwonayo Baba akifanya. Baba ndani Yangu, akinionyesha maono haya, na ndipo ninatoka ninaenda kufanya yale tu ambayo Baba aliniambia nifanye." Mnalipata? Mungu alikuwa ndani ya mwili wa kibinadamu, si nyuma ya ngozi za mbuzi zilizotiwa rangi, bali alikuwa akiishi, akitembea. Mungu alikuwa na mikono; Mungu alikuwa na miguu; Mungu alikuwa na ulimi; Mungu alikuwa na macho; na ilikuwa ni Kristo. Huyo hapo.

92 Sasa, aliondoka akaenda zake, naye Roho akaja kwa jinsi hiyo, ili kwamba kwa kifo Chake apate kulikamilisha Kanisa na kulitiisha Kanisa. Ndipo basi Roho yeye yule aliyekuwa ndani ya Kristo yumo ndani ya Kanisa, akifanya mambo yale yale Kristo aliyofanya. "Bado kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona tena; bali ninyi mtaniona, kwa maana nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari."

93 Sasa sikilizeni jambo hili.

*Lakini Kristo akiisha kuja, aliyefanyika kuhani mkuu wa mambo mema yatakayokuwapo, kwa hema iliyo kubwa na kamilifu zaidi, isiyofanyika kwa mikono, maana yake, isiyo ya ulimwengu huu,*

Hakufanywa kwa mikono. Yeye alizaliwaje? Uzazi wa kibikira.

> *Wala si kwa damu ya mbuzi na ndama, mwili huu* haukutolewa dhabihu ama kutakaswa*, bali kwa damu yake mwenyewe*. . .

94 Mnajua ya kwamba damu hutokana na jinsia ya kiume. Na basi mtu fulani alisema, "Loo, Yesu alikuwa ni Myahudi." Hakuwa Myahudi. "Loo, tunaokolewa na damu ya Kiyahudi." La, hata. Kama tuliokolewa kwa damu ya Kiyahudi, tungali tumepotea.

Yesu hakuwa Myahudi, wala Yeye hakuwa Mmataifa. Alikuwa ni Mungu: Mungu Baba, Roho, Yeye asiyeonekana. "Hakuna mtu aliyemwona Mungu wakati wowote, bali Mwana pekee wa Baba amemdhihirisha." Yeye alimdhihirisha Mungu, kile Mungu alichokuwa.

95 Sasa kanisa Lake linapaswa kumdhihirisha Mungu, kuonyesha Mungu ni nani. Unaona?

Tunafanya nini? Tunajiundia madhehebu, na "Sina uhusiano wowote nao. Hao ni Wamethodisti. Hao ni Wapresbiteri. Sitaki kuwa na uhusiano wowote. Mimi ni Mbaptisti. Mimi ni Mpentekoste." Aa! Umepotea, ukiwa na nia kama hizo. Kweli.

96 Ni nani anayeweza kujivuna? Ni nani anayeweza kusema jambo lolote? Angalia hiyo aibu waliyoileta Wapresbiteri. Angalia hiyo aibu, Wabaptisti. Angalia hiyo aibu, Wakatoliki. Angalia hiyo aibu, Wapentekoste, Wanazarayo, Wapilgrim Holiness. Waangalie hao wengine wote.

Lakini, ninawapa changamoto mnyoshee mkono, katika aibu, kwa Huyo. Naam. Nyosheni kidole, wakati Mungu Mwenyezi aliposema, "Huyu ni Mwanangu mpendwa ninayependezwa kukaa ndani Yake. Msikieni Yeye." Huyo hapo. Huyo Ndiye yule Mkamilifu.

97 Sasa, hebu na tuendelee kusoma mbele kidogo hapa sasa.

> *Wala si kwa damu ya mbuzi*. . .*ndama, bali kwa damu yake mwenyewe aliingia mara moja tu katika Patakatifu, akiisha kupata ukombozi wa milele*. . . (Mnalipata?) . . .*ukombozi wa milele* kwa ajili yetu.

98 Si kukombolewa leo, na halafu, juma lijalo ufufuo unapoanza, unakombolewa tena, na halafu, loo, tunarudi nyuma na kukombolewa tena. Unakombolewa mara moja, milele. Hiyo ni kweli. Hakuna tena kukombolewa, kukombolewa, kukombolewa. "Ukombozi wa milele!" "Yeye ayasikiaye Maneno Yangu na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa Milele, wala hataingia hukumuni, bali ame-," wakati uliopita, "-pita toka mautini kuingia Uzimani." Kwa sababu ati ametetemeka? Kwa sababu ati alibatizwa kwa njia fulani? Kwa sababu alikuwa na damu mkononi mwake? "Kwa maana

amemwamini Mwana wa pekee wa Mungu." Hivyo ndivyo tunavyokuwa na ukombozi wa Milele.

99 Sikilizeni sasa.

> *Kwa maana,. . .damu ya mbuzi na mafahali na majivu ya* ndama ya ng'ombe *waliyonyunyiziwa na—nanii. . .* kunyunyiziwa *wenye uchafu* hutakasa *hata kuusafisha mwili;*
>
> *Basi si zaidi damu yake Kristo, ambaye kwamba kwa Roho wa milele alijitoa nafsi yake kwa Mungu kuwa sadaka isiyo na mawaa,* ilitusafisha *dhamiri zetu na matendo mafu, mpate kumwabudu Mungu aliye hai?*

100 "Umepita toka mautini kuingia Uzimani." Unajali nini yale dunia iwazayo? Unajali nini yale jirani yako awazayo? Dhamira yetu imekufa, nasi tumeongoka na kuzaliwa mara ya pili kwa Roho wa Mungu, kumtumikia Mungu wa kweli na aliye hai. Haya basi.

101 Sasa shuka kwenye kifungu cha 10. . .mlango wa 10, hasa, papo hapo upande wa pili wa ukurasa huo.

> *. . .torati, kwa kuwa ni kivuli cha mema yatakayokuwa, wala si sura yenyewe ya mambo hayo, kwa dhabihu zile zile wanazozitoa kila mwaka, daima haiwezi wakati wo wote* kumfanya akaribiaye m-k-a-m-i-l-i-f-u.

M-k-a-m-i-l-i-s-h-a, liko pale, "Mkamilifu."

> *. . .tukiacha kuyanena mafundisho ya kwanza ya Kristo, tukaze mwendo ili tuufikilie utimilifu;. . .*
>
> *Basi ninyi mtakuwa wakamilifu, kama Baba yenu. . . mbinguni alivyo mkamilifu.*

102 "Torati ikiwa ni kivuli cha mema yatakayokuwa," amri zote na mabatizo na ninii. . .mambo hayo mengine yote waliyokuwa nayo, "yasingeweza kumkamilisha akaribiaye." Na, hata hivyo, Mungu anahitaji "ukamilifu."

103 Unajiunga na kanisa la Kinazarayo, halitakufanya mkamilifu kamwe. Unajiunga na kanisa la Kibaptisti, Kipentekoste, lolote lile, kamwe halitakufanya mkamilifu. Wewe kuwa mtu mzuri, mtu mwaminifu, kamwe halitakufanya mkamilifu. Huwezi kustahili hata jambo moja. Hakuna kitu kukuhusu wewe, cha kukustahilisha. Umepotea. Unasema, "Vema, nilitimiza sheria. Ninaadhimisha Sabato. Ninatimiza hili, maagizo yote ya Mungu. Ninafanya hili."

104 Paulo alisema, "Na tuweke kando mambo hayo yote sasa."

105 "Hayo ni sawa, bali tutafanya jambo *hili*. Tutawabatiza watu, na tutawawekea mikono kwa ajili ya uponyaji wao na kadhalika."

106 Tungeweza kulichukua, kifungu kwa kifungu, kila mojawapo ya mambo hayo. Ubatizo, tunauamini. "Kuna tumaini moja, Bwana mmoja, Imani moja, Ubatizo mmoja." Tunaamini ya kwamba kuna ubatizo. Tunaamini katika ufufuo wa wafu. Kweli kabisa. Tunaamini Yesu alikufa na kufufuka tena. Tunaamini mambo hayo. "Kuwekea mikono, kwa ajili ya wagonjwa," hivyo ndivyo lilivyosema. "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya." Tunaamini hilo.

Lakini hilo ni nini? Paulo alisema, "Zote ni kazi zilizokufa." Ni jambo fulani unalofanya.

107 "Sasa na tukaze mwendo ili tuufikilie utimilifu." Loo, jamani! Tunaingia katika ile Maskani, si kwenye msingi; Maskani, Maskani Yenyewe. Hiyo ndiyo msingi: torati, na haki, na—na—na—na kujiunga na kanisa, na kubatizwa, na—na kuwekea mikono. Hayo yote ni taratibu za kanisa.

"Lakini sasa na tukaze mwendo ili tuufikilie utimilifu." Na kuna Mmoja tu aliye mkamilifu, huyo ni Yesu.

108 Tunaingiaje ndani Yake? "Kwa kupitia kwa Wamethodisti?" La. "Mpentekoste?" La. "Kuwa Mbaptisti?" La. "Kwa kupitia kwenye kanisa lolote?" La. "Katoliki la Kirumi?" La.

109 Tunaingiaje ndani Yake? Warumi 8:1.

> *Sasa, basi, hakuna hukumu ya adhabu juu yao walio katika Kristo . . . wanaoenenda si kulingana na mambo ya dunia hii, mwili, bali kulingana na mambo ya Roho, wasiojali yale ulimwengu unayosema.*

110 Hata kama wewe ni mgonjwa, daktari anasema, "Utakufa," hujali jambo hilo, halikusumbui hata kidogo.

111 Kama wakikwambia, "Inakubidi kuwa Mkatoliki kabla hujaokoka, ama Mpresbiteri, ama inakubidi kufanya jambo hili," hujali jambo hilo.

"Kwa hiyo hakuna hukumu ya adhabu juu yao walio katika Kristo Yesu, wanaoenenda si kulingana na mapenzi ya mwili, mambo wanayoona." Kila kitu unachoona kwa macho yako ni cha duniani.

112 Lakini ni mambo yale unayoona kwa roho yako, kupitia Neno! Neno ni kioo cha Mungu cha kujiangalia ambacho huakisi kile alicho Yeye na kile ulicho wewe. Haleluya! Loo, jamani! Linakwambia. Hiki ndicho Kitabu pekee ulimwenguni kinachokwambia unakotoka, kwamba wewe ni nani, na mahali unakoenda. Nionyeshe ukurasa wowote wa vitabu mbalimbali, mahali popote, pamoja na sayansi yote ama chochote kile, kila kitabu kizuri kilichowahi kuandikwa, hakuna hata kimoja cha hivyo kinachoweza kukwambia jambo hilo. Hiki ni kioo cha Mungu cha kujiangalia, ambacho kinaonyesha kwamba Yeye ni nani na kwamba wewe ni nani. Halafu, pale katikati kuna mstari

wa Damu, unaoonyesha kile unachoweza kuwa kama ukifanya chaguo. Haya basi.

113 "Kwa Roho mmoja," sasa, Wakorintho wa Kwanza 12. Tunaingiaje katika Mwili huo?

"Kwa kupeana mikono?" La, bwana. "Kwa kujiunga na kanisa?" La, bwana. "Kwa kubatizwa kichalichali, kifudifudi? Katika jina la Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu? Jina la Yesu Kristo? Jina la Ua la Uwandani, Ninyoro ya Bondeni, Nyota ya Asubuhi? Lolote unalotaka?"

Hilo halina uhusiano wowote nalo. "Ni jibu tu la dhamiri safi mbele za Mungu." Na hata hivyo tunakerana, na kuzozana, na kubishana, na kutengana, na kutofautiana. Hiyo ni kweli. "Lakini hayo yote ni matendo mafu." Tunaelekea kwenye utimilifu.

114 Hayo ni mambo niliyofanya. Mhudumu alikubatiza. Iwapo alikubatiza kifudifudi, kichalichali, ama mara tatu, mara nne, ama mara moja, ama vyovyote alivyofanya jambo hilo, hilo halina uhusiano Nalo. Umebatizwa tu ukaingizwa katika ushirika wa kanisa hilo, hata hivyo, ukilithibitishia kanisa hilo: unaamini mauti, kuzikwa, na kufufuka kwa Kristo. Kuwekea mikono, kuwaponya wagonjwa, hayo ni mambo mazuri sana, lakini, hayo yote ni mambo ya mwilini, na mwili huo utakufa tena kwa uhakika tu kama unavyoishi. Utakufa tena. "Sasa na tuweke kando mambo hayo yote, na tukaze mwendo tuufikilie utimilifu."

115 Tunaufikiliaje utimilifu? Hivyo ndivyo tunavyotaka kujua.

. . . Kristo *amekamilisha* . . .

"Mungu aliweka juu yake maovu yetu yote. Alijeruhiwa kwa makosa yetu, alichubuliwa kwa maovu yetu, adhabu ya amani yetu ilikuwa juu Yake, kwa mapigo yake sisi tuliponywa." Huo ndio Mwili tunaotaka kuufikia. Huo ndio ule Mwili. Kwa nini? Kama uko ndani ya huo Mwili, hutaona hukumu kamwe, hutaonja mauti kamwe. Uko huru na mambo yote ya kufa, hukumu, dhambi, na chochote kile, unapokuwa katika Mwili huo.

116 "Unauingiaje, katika Huo ewe mhubiri? Kwa kujiunga na maskani hii?" Umepotea, bado. Usingeweza kujiunga, hata hivyo; hatuna kitabu chochote. "Tunauingiaje? Kwa kujiunga na kanisa fulani?" La, bwana. "Unaingiaje ndani Yake?" Unazaliwa ndani Yake.

117 Wakorintho wa Kwanza 12.

*Kwa maana katika Roho mmoja sisi sote tulibatizwa kuwa mwili mmoja, . . .*

118 Kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu, tunabatizwa katika Mwili Huo, na tuko huru na dhambi. Mungu hakuoni tena; Yeye anamwona Kristo pekee. Na unapokuwa katika Mwili

huo, Mungu hawezi kuuhukumu Mwili huo. Yeye tayari ameuhukumu. Alichukua hukumu zetu na kutualika tuingie ndani. Na kwa imani, kwa njia ya neema, tunaingia, tunakubali msamaha wetu. Ndipo Roho Mtakatifu anatuingiza katika ushirika huu pamoja Naye. "Ndipo hatutembei tena kwa mapenzi ya mambo ya ulimwengu, bali tunatembea katika Roho."

Tumehuishwa, Neno lilitujia. Yeye alikufa mahali pangu. Nimefanywa hai. Mimi hapa, ambaye kwanza nilikuwa nimekufa katika dhambi na makosa, nikafanywa hai. Shauku zangu zote ni kumtumikia Yeye. Upendo wangu wote ni Kwake. Mienendo yangu yote ni kutaka iwe katika Jina Lake. Kokote niendako, chochote nifanyacho, ninamtukuza Yeye. Kama ninawinda, kama ninavua samaki, kama ninacheza mpira, na lolote nifanyalo, sina budi kuwa, "Kristo ndani yangu," katika maisha ambayo, yatawafanya watu watamani kuwa hivyo, si kupiga domo, kusengenya, na kuzozana juu ya makanisa yenu. Mnalipata? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

"Kwa Roho Mmoja tumebatizwa kuwa Mwili huo." "Na nitakapoiona Damu hiyo, nitapita juu yenu."

119 Sikilizeni. Hebu na tusome mbele kidogo tu hapa, tafadhalini.

> . . . kile kisichoweza *kumkamilisha* akaribiaye.

Kwa kifungu cha 2, mlango wa 10.

> *Kama ndivyo, je! dhabihu* hazingekoma *kutolewa?*

120 Kama hizo zingeweza kumkamilisha mtu . . . Na Mungu anataka ukamilifu. Kama kushika torati, kama kutimiza amri zote, kungekukamilisha wewe, basi hakuna—hakuna haja ya kuwa na kitu kingine chochote; wewe tayari umekamilishwa. Maana, unapokuwa mkamilifu, wewe ni wa Milele. Maana, Mungu ndiye pekee aliye wa Milele, na Mungu ndiye tu aliye mkamilifu. Na njia pekee unayoweza kuwa wa Milele, ni kufanyika sehemu ya Mungu. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

> *. . . wakiisha kusafishwa mara moja, wasingejiona tena kuwa na dhambi?*

Ati nini? "Mwabuduo akiisha kusafishwa mara moja, asingejiona tena ana *dhamira* ya kuwa na . . . " Kama ukiandika fasiri ya hilo, ni "shauku."

> . . . mwabuduo *akiisha kusafishwa mara moja, . . . asingejiona tena kuwa na* shauku *ya dhambi?*

> *. . . kama mwabuduo* aliisha *kusafishwa mara moja, . . .*

121 Unaenda juu sasa na kusema, "Loo, haleluya, niliokoka jana usiku. Lakini, vema, Mungu abarikiwe, *mwanamke* mmoja

alinifanya nirudi nyuma. Haleluya, siku moja nitaokoka tena." Ewe maskini mjinga usiyefunzwa. Hivyo sivyo ilivyo.

122 "Mwabuduo akiisha kusafishwa mara moja asingejiona tena kuwa ana dhambi," Biblia ilisema. Sikiliza, tunapoendelea kusoma, kwa dakika moja tu.

> *Lakini katika dhabihu hizo*. . .kama zinavyokumbukwa dhidi ya dhambi kila mwaka.

123 Sasa tutashuka chini, tugusie kwenye kifungu cha 8, kuokoa wakati, na mahali ninapotaka kufikia.

> *Hapo juu basi asemapo, Dhabihu na matoleo na sadaka za kuteketezwa*. . .*hizo za dhambi hukuzitaka, wala hukupendezwa nazo (zitolewazo kama ilivyoamuru torati,)*

124 Kifungu cha 9.

> *Ndipo aliposema, Tazama, nimekuja niyafanye mapenzi yako, Ee Mungu. Aondoa la*. . .*ondoa*. . . *Aondoa la kwanza, torati, ili kusudi alisimamishe la pili.*

125 Laiti tungalikuwa na wakati wa kukaa kwenye jambo hilo. Mradi tu wewe ni Mpresbiteri, ama Mpentekoste, ama Mbaptisti, ama Mmethodisti, Yeye kamwe hawezi kufanya jambo lolote nawe. Hana budi kuondolea mbali hayo yote, kwanza, unaona, kusudi apate kusimamisha la pili. Mradi tu unasema, "Vema, mimi ni Mmethodisti." Aa, sina kitu dhidi ya Wamethodisti, wala Wabaptisti, wala Wapentekoste. Lakini, ndugu, hilo halininii—hilo halimaanishi kitu. Inakupasa kukaza mwendo kuufikilia utimilifu, yaani kuingia katika Kristo.

126 Angalia jambo hili sasa, kwa dakika moja tu.

> *Katika mapenzi hayo tumepata utakaso, kwa kutolewa mwili wa Yesu Kristo mara moja tu.*

127 Aa? Hebu na tuendelee tu kusoma mbele kidogo, na mlishikilie hilo. Hebu hilo na likolee wakati tunaposoma, "Mara hii tu."

> *Na kila kuhani husimama kila siku akifanya ibada, na kutoa dhabihu zile zile mara nyingi; ambazo haziwezi kabisa kuondoa dhambi.*
>
> *Lakini mtu huyu*. . .

Mko tayari? Mmefungua vizibao vyenu sasa, kusudi lisiwapige chenga, litaingia moja kwa moja moyoni? "Lakini Mtu huyu." Mtu gani? Si papa wa Roma, si askofu wa kanisa la Kimethodisti, wala wa kanisa lingine lolote.

> *Lakini mtu huyu, Kristo, alipokwisha kutoa kwa ajili ya dhambi dhabihu moja idumuyo hata milele, aliketi mkono wa kuume wa Mungu;*

*Tangu hapo akingojea hata adui zake wawekwe kuwa chini ya miguu yake.*

Angalia. Hili hapa linakuja.

*Maana kwa toleo moja* a-m-e-w-a-k-a-m-i-l-i-s-h-a, *amewakamilisha . . .*

"Mpaka ufufuo ujao"? Hilo lingesema nini?

*. . . amewakamilisha hata milele hao wanaotakaswa.*

Mnalipata? "Na tukaze mwendo tuufikilie utimilifu."

128 Sasa ninyi watu wa utakatifu mnasema, "Loo, naam, tunaamini katika utakatifu. Haleluya! Tunaamini katika kutakaswa." Lakini mnachukua mambo yenu wenyewe. Mnaacha tu hili na kuacha lile. Mnajua hampaswi kulifanya.

Kristo asipoufungua mlango na kulihuisha moyoni mwako, nawe unafikia mahali ambapo dhambi imekufa, na tamaa, yote yamekufa. Basi, Yeye anaondoa haki yako wewe mwenyewe, apate kufanya makao ndani yako. "Na huyo ni Kristo, Mwana wa Mungu, ndani yako, tumaini la Utukufu."

*. . . tukaze mwendo tuufikilie utimilifu;*

129 Tunawezaje kuwa wakamilifu? Kwa mauti ya Kristo. Si kwa kujiunga na kanisa. Si kwa matendo yetu mema, yale tunayofanya. Hayo yote ni sawa. Si kwa sababu ati tulibatizwa *hivi* ama *vile*. Si kwa sababu kwamba eti tumeponywa, kwa kuwekewa mikono. Si kwa sababu ya yoyote ya mambo haya mengine, "Tunaamini katika kifo, kuzikwa, na kufufuka."

130 Paulo alisema, "Ningeweza kunena kwa lugha za wanadamu na za Malaika," hizo ni lugha zinazoweza kueleweka na zile zisizoweza kueleweka, zinazopaswa kufasiriwa, "si kitu mimi. Nijapokuwa na karama ya maarifa na kufahamu hekima yote ya Mungu," ninaweza kuielezea Biblia, kutoka . . . kuifunganisha pamoja, "si kitu mimi." Haisaidii sana kwenda shuleni basi, sivyo, kujifunza Biblia? "Nijapokuwa na imani hivi kwamba naweza kuhamisha milima . . . " Kampeni za uponyaji hazina faida sana basi, sivyo? "Si kitu mimi, nijapotoa mwili wangu niungue moto kama dhabihu."

131 "Loo," wao wanasema, "mtu yule ni wa kidini."

132 "Lakini yeye si kitu," Paulo alisema, "hakuwa kitu hata kidogo."

133 "Kwa maana palipo na lugha, zitakoma; palipo na unabii, utabatilika; palipo na mambo haya mengine yote, yatabatilika. Lakini ijapo ile iliyo kamili, iliyo kwa sehemu itabatilika." Unaona, ile iliyo "kamili." Ni nini iliyo kamili? Upendo. Upendo ni nini? Mungu. "Na tuweke kando kazi hizi zote ndogo zilizokufa na sheria za ibada, na tukaze mwendo tuufikilie utimilifu." Mnaona jambo hilo? Tunakamilishwa kwa njia

ya Kristo. Tunaingiaje ndani Yake? Kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu.

134 "Vema, inakuwaje?" Umepita toka mautini ukaingia Uzimani.

135 "Vema, je! inatakiwa nitetemeke, niruke, nifanye jambo hilo?" Wewe, wewe haitakubidi kufanya lolote. Umelifanya tayari, Mungu alikutoa mautini akakuingiza Uzimani, nawe uko hai. Ndipo matunda ya maisha yako yanaonyesha jambo hilo.

136 Wengi wenu ninyi Wamethodisti na Wanazarayo mlipaaza sauti kwa nguvu tu mlivyoweza kupaaza, mtu akaiba mahindi kutoka kwenye shamba la mtu, hiyo ni kweli, mnafanya kila kitu ambacho kingaliweza kufanywa.

137 Wengi wenu ninyi Wapentekoste mlinena kwa lugha, kama kumwaga mbaazi juu ya ngozi ya ng'ombe, hakika, mkatoka mkaenda moja kwa moja na kumtorosha mke wa mtu mwingine, mkafanya mambo ya kila namna. Hilo silo, ndugu.

138 Msijaribu kupata mhemuko wowote wala chochote kile kipachukue mahali pa Roho Mtakatifu. Kuzaliwa kupya kunapokuja, unabadilishwa. Haikubidi kufanya jambo lolote kuthibitisha jambo hilo. Maisha yako yanalithibitisha, unapotembea. Wewe ni upendo, amani, uvumilivu, utu wema, upole, subira. Hivyo ndivyo ulivyo, na ulimwengu mzima unaona sura ya Yesu Kristo ndani yako.

139 Sasa, kunena kwa lugha, huko kupaaza sauti, hizo ni tabia tu zinazofuatana na Maisha ya namna hii.

Nawe unaweza kuchukua, kuiga tabia hizi, wala kamwe usiwe na Maisha hayo. Tunaona jambo hilo. Ni wangapi wanaojua ya kwamba hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Hakika, mnajua. Hakika, bila shaka mnajua hivyo. Jamani! Mnaliona jambo hilo mahali pote mlipo.

140 Kwa hiyo, hakuna kitu unachoweza kusema ni thibitisho la Roho Mtakatifu, isipokuwa iwe ni maisha yako unayoishi. Sasa, kama ukitaka kunena kwa lugha, hilo ni sawa kabisa kama unaishi maisha yanayounga jambo hilo mkono. Hilo ni sawa. Na kama unataka kupiga makelele, sawa, hilo ni sawa. Mimi ninapaaza sauti, pia, ninakuwa na furaha sana mara nyingine hata siwezi kuvaa jozi ya viatu; ninajisikia kama niruke nitoke ndani yake. Na hilo ni zuri sana. Ninaliamini.

141 Nimeona maono, na wagonjwa wakiponywa, na wafu wakifufuliwa. Wakati wamelala pale na madaktari wanaondoka zao na kusema, "Wamekwisha na wameaga dunia," wanabaki pale kwa saa kadhaa; ndipo Roho Mtakatifu anashuka moja kwa moja na kuonyesha ono, ninashuka ninaenda kule na kumfufua mtu huyo. Nimeona hao walio viziwi, bubu, na vipofu, na viwete, wakitembea. Hilo halininii . . . Hizo ni sifa tu.

142 Ndugu, zamani za kale, kabla ulimwengu haujawekwa msingi; Mungu kwa neema Yake ya Milele, aliangalia chini, na kwa kutangulia kujua alikuona wewe na mimi. Alijua kwamba tungeishi katika wakati gani. Alijua kile tungekuwa. Kwa hiyo, kwa kuteuliwa, Yeye alituchagua kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, tuwe pamoja naye bila waa.

143 Sasa, kama Yeye alituchagua kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu tuwe ndani Yake bila waa, nasi tunazaliwa tumejaa mawaa, wala hakuna kitu kingine kinachoweza . . . hakuna kinachoweza kutusafisha, tutakuwaje bila . . . tutakuwaje bila waa? "Yeye alimtuma Mwanawe wa pekee, ili kila amwaminiye asiwe na mwisho wa uhai wake, bali awe na Uzima wa Milele; asipotee kamwe, bali awe na Uzima wa Milele." Ndipo tunapokuja kuingia ndani Yake, kwa imani, kwa neema tunaokolewa, kwa kuitwa na Roho Mtakatifu.

144 Kabla hapajakuwapo na mwili katika dunia hii, miili yenu ilikuwa inakaa hapa. Imefanyizwa kwa kalisi, potashi, unyevu, miali—mialimwengu, na petroli, na kadhalika, elementi kumi na sita. Ndipo Roho Mtakatifu akaanza kuatamia juu ya nchi, "kubembeleza." Na alipofanya hivyo, muda si muda wajua, ua dogo la Pasaka likachipuka. Ndipo akaatamia nyasi, na ndege, na baada ya muda kidogo, mtu akatokea.

145 Sasa, kamwe hakumfanya mwanamke kutoka katika mavumbi ya ardhi. Yeye tayari ni mwanamume, kwanza; mwanamume na mwanamke ni mmoja. Kwa hiyo Yeye alitoa kutoka katika ubavu wa Adamu, ubavu, na akamfanya mwanamke, msaidizi wa mwanamume. Na ndipo dhambi ikaingia. Basi baada ya dhambi kuingia . . .

146 Mungu hatashindwa, hata jambo gani litukie. Yeye kamwe hatashindwa. Ndipo, wanawake wakaanza kuzaa wanaume duniani. Naye Mungu, kwa neema ya Milele, aliona ni nani angeokolewa, ndipo akakuita. "Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu, asipovutwa na Baba Yangu, kwanza." "Si katika uwezo wa yule atakaye, wala wa yule apigaye mbio, bali wa yule arehemuye, yaani, Mungu."

147 Unasema, "Vema, nilimtafuta Mungu. Nilimtafuta Mungu." La, hukumtafuta. Mungu alikutafuta. Hivyo ndivyo ilivyokuwa hapo mwanzo.

148 Haikuwa ni Adamu akisema, "Ee Baba, Baba, nimefanya dhambi. Uko wapi?"

149 Ilikuwa ni Baba akisema, "Ee Adamu, Adamu, uko wapi?" Hiyo ndiyo tabia ya mwanadamu. Hayo ndiyo maumbile ya mwanadamu. Hivyo ndivyo alivyotengenzwa

150 "Wala hakuna mtu awezaye kuja Kwangu asipovutwa na Baba Yangu. Na wote anaonipa Baba . . ." Haleluya! "Wote wanijiao, nitawapa Uzima wa Milele, nami nitamfufua katika siku ya mwisho." Ni yenye baraka, ni ahadi yenye baraka jinsi

gani, ya Mungu wa Mbinguni! Mahali tutakapofikia usiku wa leo, ambapo, "Aliapa kwa nafsi Yake." Hakuna aliye mkubwa zaidi. Unaapa kwa mtu aliye mkuu kuliko wewe. Hapakuwapo na aliye mkuu zaidi, kwa hiyo Mungu aliapa kwa nafsi Yake. Tunaliingilia jambo hilo, jinsi alivyofanya jambo hilo na wakati alipolifanya hilo; na akaapa kwa nafsi Yake, ya kwamba atatufufua na kutufanya urithi Wake mwenyewe.

151 Loo, jinsi tunavyoweza kusimama kikamilifu na imara, asubuhi ya leo! Jinsi unavyoweza kuangalia, kama mauti inakukazia macho moja kwa moja usoni, ungeweza kusema kama Paulo, "Mauti, u wapi mwiba wako? Kaburi, u wapi ushindi wako? Bali Mungu na ashukuriwe, atupaye ushindi kwa Bwana wetu Yesu Kristo." Haya basi. Kwa nini?

152 "Loo, ulifanya *hivi na hivi*."

153 "Ninajua jambo hilo, lakini nimefunikwa na Damu Yake." Haleluya!

154 "Kwa Roho mmoja, sisi sote tulibatizwa kuwa Mwili mmoja." Ninyi Wamethodisti, Wabaptisti, Wapresbiteri, lolote uwalo, tulibatizwa kuwa Mwili mmoja. Tuna ushirika, nasi ni raia wa Ufalme wa Mungu, tukikiri, ya kwamba, "Sisi si wa ulimwengu huu."

155 Maskini msichana wangu mdogo alikuja, hivi majuzi, akasema, "Baba, maskini msichana huyu mdogo alifanya *hivi na hivi*. Na watu fulani walifanya *hivi na hivi*. Tulienda kwenye nyumba. Walifanya *hivi na hivi*." Nikasema . . . Kasema, "Kwa nini sisi tusifanye hivyo?"

156 Nikasema, "Kipenzi, sisi si wa ulimwengu huo. Wao wanaishi katika ulimwengu wao wenyewe."

157 Kasema, "Kumbe hatutembei juu ya ardhi ile ile?"

158 Nikasema, "Wa ulimwengu, kipenzi. Sisi si wa hao watu."

159 Biblia ilisema, "Tokeni kwake, mkatengwe nao," asema Mungu. Unaona, wewe si wa aina hiyo. Na hapo Asili hiyo mpya inapoingia ndani yako, haikulazimu kuvutwa utoke. Hutaki kurudi, kama mke wa Lutu. Umezaliwa tu, kutoka katika hiyo. Nawe uko kwenye kiwango kingine. Na kiwango chao kinaonekana ni upuuzi kwako.

Nayo hii, Marekani kuu, inayosifika tunamoishi, imekuwa mchafuko mmoja mkubwa wa mambo. Kila kitu ni ashiki na wanawake. Na wanawake jinsi wanavyovalia, wanaume jinsi wanavyoenenda, na—na mambo wanayofanya, na halafu wanajiita wenyewe "Wakristo."

160 Kwa mfano, huyu Elvis Presley, ameenda na kujiunga na kanisa la Kipentekoste sasa. Kwa kweli, huko ndiko Yuda alikopata vipande thelathini vya fedha. Elvis alipata mlolongo wa kadilaki, na do-—na dola milioni kadhaa, kwa kuuza haki yake ya mzaliwa wa kwanza. Arthur Godfrey. Angalia hilo.

161 Mwangalie Jimmy Osborne kule Louisville, yuko huko akiwa na uchafu huo wa bugibugi, roki, upuuzi mtupu mchafu na kinyaa. Na Jumapili asubuhi, anachukua Biblia na kusimama jukwaani na kuhubiri. Ni fedheha jinsi gani!

Si ajabu Biblia ilisema, "Kila meza imejaa matapiko." Mbona, tunaishi katika siku za kutisha sana!

162 Nao watu wanasema, "Loo, wao ni wa kidini sana." Loo! Hivi hujui ya kwamba Ibilisi ni mshika dini sana? Hivi hujui ya kwamba Kaini alikuwa ni wa kidini tu kama vile Habili alivyokuwa? Lakini, hakuwa na Ufunuo. Hivyo ndivyo ilivyo. Hakuwa na Ufunuo.

Naam, sote huenda kanisani, bali kuna wengine walio na Uzima, hao ndio wale walio na Ufunuo wa Yesu Kristo moyoni mwao. Si kwa kutetemeka, kuruka, si kwa kujiunga na kanisa. Bali, Ufunuo, Mungu amemfunua Yeye.

163 Angalia yale aliyosema, "Watu husema Mimi, Mwana wa Adamu, kwamba ni nani?"

164 "Wengine walisema Wewe ni 'nabii fulani.' Na wengine wanasema Wewe ni 'Eliya.' Na wengine . . . "

Kasema, "Lakini ninyi mnasema ni nani?"

165 Petro alisema, "Wewe ni Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai." Hilo halikutoka kinywani mwake.

166 Akasema, "Heri wewe, Simoni, mwana wa Yona, kwa kuwa mwili na damu havikukufunulia hili. Hukujifunza hili katika maadili fu—fulani ya Biblia, wala seminari fulani za theolojia. Heri wewe, kwa kuwa mwili na damu havijakufunulia hili. Bali Baba Yangu aliye Mbinguni amekufunulia hilo. Na juu ya mwamba huu nitalijenga Kanisa Langu, na malango ya kuzimu hayawezi kulishinda."

167 Kama wewe ni Mkristo, asubuhi ya leo, kwa kuwa wewe ni mfuasi wa kanisa, umepotea. Kama wewe ni Mkristo kwa sababu umepita toka mautini ukaingia Uzimani, uko huru na hukumu; ukaingia katika Kristo, unafikia utimilifu wakati wote. Mungu hawezi kuona hata jambo moja. Unasema, "Vema, hivi nitakuja kufanya kosa lolote?" Hakika, bali hulifanyi makusudi.

168 Sasa tunafikia jambo hilo, mnamo dakika chache tu, "Kwa kuwa yeye anayetenda dhambi makusudi baada ya kupokea ujuzi wa Kweli, hakuna tena dhabihu ya dhambi." Tutafikia jambo hilo usiku wa leo, kwa maana kidogo wakati umeenda sana sasa.

169 Hebu na tusome baadhi ya vifungu vingine vichache zaidi vya hili, tupate kujisikia vizuri zaidi juu ya kuendelea chini kidogo zaidi. Sawa. Vema, tutaanzia papo hapo usiku wa leo, kifungu cha 4. Sikilizeni jambo hili.

*Kwa maana hao waliokwisha kupewa nuru, na* kufanywa*. . .na* wameninii*. . .na kukionja kipawa cha mbinguni, na kufanywa washirika wa Roho Mtakatifu,*

*Na kulionja neno zuri la Mungu, na nguvu za zamani zijazo,*

*Wakaanguka baada ya hayo, haiwezekani kuwafanya upya wenyewe. . .hata wakatubu,. . .*

Unaona? Na tunachukua hilo tunaliingiza kwenye Waebrania 10, na huku na huko kuonyesha kwamba hii ni nini.

170 Wapendwa, "Na tukaze mwendo tuufikilie utimilifu." Tumeninii. . .sisi si. . .Hatuna udhuru leo. Hatuna udhuru, hata kidogo. Mungu wa Mbinguni ameonekana katika siku hizi za mwisho na anafanya mambo yale yale aliyofanya wakati huo, wakati alipokuwa hapa hapo awali, alipokuwa hapa duniani. Amethibitisha, kama vile tunavyopitia kwenye Biblia hii. Nanyi—ninyi, darasa, mnajua jambo hili, ya kwamba tumechukua muujiza kwa muujiza, ishara kwa ishara, na ajabu kwa ajabu, aliyofanya na wale wana huko jangwani, mambo na ishara alizofanya; mambo aliyofanya wakati alipokuwa hapa duniani, akadhihirishwa katika mwili; na mambo yayo hayo yanatukia siku hizi, papa hapa miongoni mwetu. Hili hapa Neno kuthibitisha jambo hilo. Hiki hapa kitu hicho kusema kwamba ni kweli, kulifanya ni kweli. Huyu hapa Roho wa Mungu kufanya jambo lile lile, kwa hiyo hatuna udhuru.

Na tuombe.

171 Baba wa Mbinguni! Kwa kuwa tumezungukwa na wingu kubwa la mashahidi namna hii, na tuweke kando kila neno, kila kitu, kila kosa, kila neno baya, kila neno lililonenwa vibaya, kila wazo, "na tupige mbio kwa saburi katika yale mashindano yaliyowekwa mbele yetu, tukimtazama mwenye kuanzisha na mwenye kutimiza imani yetu, Bwana Yesu Kristo." Ee libarikiwe Jina Lake takatifu na lisilo na kifani! Jinsi ambavyo alikuja duniani kumkomboa mwanadamu aliyeanguka, na kuwarudisha katika ushirika wa Bwana Mungu. Nasi tunakushukuru kwa ajili ya jambo hili. Na sasa kwa neema Yake. . .Hatukumchagua kamwe, bali Yeye alituchagua. Yeye alisema, "Hamkunichagua Mimi, bali Mimi niliwachagua." Lini? "Kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu."

172 Na, Mungu mpendwa, kama kuna wengine wanaoketi hapa asubuhi ya leo, ambao labda wameahirisha jambo hili kwa miaka kadha wa kadha, bali daima kuna kubisha kudogo moyoni. Labda walijiunga na kanisa, wakiwazia, "Vema, itakuwa ni sawa." Baba, hakika, Maandiko yemeelezea jambo hilo asubuhi ya leo: ya kwamba huwezi kujificha nyuma ya kanisa, na uwe mwenye haki; wala huwezi kuwa mzuri, usiseme uongo wala kuiba na kufanya jambo lolote baya, na ungali uwe ni mwenye haki.

173 Kuna haki moja tu tuliyo nayo, si yetu wenyewe, bali ni haki Yake. Yeye amekamilisha wokovu wetu. Kwa hiyo, tukiwa ndani Yake, Mungu haoni makosa yetu. Tunapofanya kosa lolote, kuna roho ndani yetu inayopaaza sauti, "Ee Baba, nisamehe!" Ndipo Mungu haoni jambo hilo. Ni . . . Tunaingizwa katika ushirika na neema pamoja Naye. Tujalie hayo, Bwana, tunapoifunga ibada hii, katika Jina la Kristo. Amina.

174 Hebu kwa muda kidogo tu, ninataka kuwauliza. Haidhuru unafanya nini, umepotea. Sikiliza jambo hili. Wakati fulani zamani . . . Huenda nililisimulia hilo hapo awali. Hili hapa tukio dogo lililonipata.

175 Nilikuwa huko To—Toledo, Ohio. Nilikuwa kwenye ufufuo na—na nikiendesha mkutano sehemu hizo na watu walikuwa ni wengi sana. Hao watu walijua zile hoteli nilizozoea; kwa hiyo walinichukua wakanipeleka kijijini. Nilikuwa nikikaa kule, kwenye moteli ndogo.

176 Tulikuwa tukila kwenye mkahawa mdogo wa Dunkard. Palikuwa ni mahali pazuri sana, hao maskini mabibi pale walionekana ni Wakristo na ni watakatifu walivyoweza kuwa, wasafi na wenye hisani. Jumapili ilifika, nikashikwa na njaa. Nilikuwa nikifunga kidogo. Nami ninataka kuvuka barabara niende kwenye nyingine, nikaagize ninii kidogo. Barabara ndogo pale pembeni, na palikuwapo na mahali maalum padogo pa kawaida, pa Kimarekani pale, pa kulia. Padogo, palikuwapo na mahali padogo, mkahawa, pako wazi usiku kucha. Nilipoingia pale Jumapili hiyo, yapata saa nane alasiri, kabla sijashuka kwenda kuhubiri alasiri hiyo.

177 Nilikuwa nimechoka sana, sikujua la kufanya. Nikaingia, na jambo la kwanza nililoona lilikuwa ni msichana mdogo mwenye umri wa miaka kumi na sita hivi, kumi na minane, kipenzi cha baba fulani, kipenzi cha mama fulani, amesimama pale nyuma pamoja na mvulana, amemkumbatia kiunoni. Kundi la matineja wameketi pale kwenye—kwenye kaunta.

178 Nikasikia mtambo wa kuchezea kamari. Nikaangalia upande *huu*, na kulikuwako na polisi mmoja amesimama pale amemkumbatia mwanamke mmoja, hapa juu, kiunoni mwake, na huku akicheza mtambo wa kamari. Sasa, mnajua kucheza kamari na mtambo wa kamari ni haramu huko Ohio, ninyi watu wa Buckeye hapa. Na mnajua jambo hilo si halali. Na hapa alikuwapo mtu mwenye kulinda sheria, akicheza mtambo wa kamari; na ni mtu wa rika yangu, labda ameoa, na ana watoto kadhaa, labda ni babu. Polisi, aliyelinda doria, akicheza kamari kwa mtambo. Kulikuwako na yule ninii kijana . . . Huyo tineja amefanya nini? Huyu amefanya nini?

179 Nilisimama pale. Hakuna mtu aliyeniona nikiingia, walikuwa wamezama katika shughuli zao, nusu yao wamelewa. Kwa hiyo, nikaangalia. Nikamsikia mtu akisema, "Vema, je!

unafikiri mvua itaathiri rubabu?" Ndipo nikageuka nikaangalia upande huu, na hapa palikuwapo na bibi mmoja ameketi pale, bibi kizee, ninii sana...Alikuwa na umri wa miaka sitini na mitano, sabini, karibu na hiyo. Na maskini bibi huyo... Simlaumu mtu yeyote kwa kuvaa vizuri sana. Lakini wakati yeye...Alikuwa amejipodoa, amezitia nywele zake rangi ya bluu, zinaonekana bluu hasa. Kisha amezipunguza zote, hapa juu, na kuzikoleza rangi ya bluu sana. Naye alikuwa amejipodoa sana kwa rangi za makucha, ama vyovyote mnavyoviita vitu hivyo alivyojipodoa navyo usoni, na ana mabaka makubwa. Naye alikuwa na kijikaptura kifupi sana, na maskini kizee hicho kilikuwa kimejaa makunyanzi mpaka nyama, legelege, nyama zilikuwa zimetepwereka namna hiyo kwenye miguu yake. Naye alikuwa amelewa. Alikuwa ameketi pale na mzee mmoja, katika wakati wa kiangazi, mzee huyo akiwa amevaa moja ya haya makabuti ya kale ya kijivu ya wanajeshi, ama ya hudhurungi iliyofifia. Lilikuwa limening'inia namna hiyo, na amevaa skafu kubwa shingoni mwake. Wamelewa, wawili wao, nao walikuwa wamemganda maskini mwanamke huyu kizee.

180 Nilisimama pale na kuangalia huku na huko. Nikasema, "Mungu, unawezaje kuvumilia jambo hilo? Nini—nini... Unaangaliaje kitu kama hicho? Wakati, kinanifanya mimi, mwenye dhambi aliyeokolewa kwa neema, kuwazia namna hiyo, unawezaje—unawezaje kuliangalia? Mbona, inaonekana kana kwamba ungeweza kukifumua kitu hicho. Je! maskini Rebekah wangu na Sarah itawabidi wakulie chini ya athari ya aina hiyo? Je! itawabidi maskini wasichana wangu wawili wadogo wakabiliane na ulimwengu wa—wa anasa, kama unaojulikana jinsi hiyo, jinsi ulivyo siku hizi, ambapo watu wanafanya hivyo? Mungu, ninawezaje...nifanye nini?"

Bila shaka, ni neema Yake. Kama walikusudiwa Uzima wa Milele, wataujia. Kama hawakukusudiwa, hawatakuja. Sijui. Hilo ni la Mungu. Nitatekeleza sehemu yangu.

181 Nikawazia, "Unawezaje kulivumilia jambo hili, Mungu? Inaonekana kana kwamba Wewe ni mtakatifu sana hata utafagilia mbali kitu hicho kitoke duniani." Nikasema, "Mwangalie maskini yule bibi aketiye pale. Mwangalie maskini msichana yule mdogo pale nyuma. Na huyu hapa mwanamke amesimama hapa, labda mwenye umri wa miaka ishirini na mitano. Na yule polisi anayemkumbatia kiunoni, akicheza bahati nasibu kwenye mtambo. Halafu hiyo hapo eti ndiyo sheria; taifa hili limekwisha. Huo hapo umama ambao umekwisha. *Huu* hapa uzee ambao umekwisha. Na yule pale maskini msichana mdogo ameketi pale nyuma, naye amekwisha. Waangalie hao wavulana, wakati wanapaswa kuwa wako kanisani ama mahali fulani."

182 Nikasema, "Ee Mungu, nifanye nini? Nami niko hapa katika mji huu, nikikemea kwa moyo wangu wote, nao wanalipuuza

na kutembea kana kwamba walikuwa. . . ” Nikawazia, “Vema, Mungu?”

183 Vema, ndipo wazo fulani likanijia, “Ikiwa Mimi sijawaita, wanawezaje kuja? Wote alionipa Baba watanijia. ‘Mna macho hata hivyo hamwezi kuona, maskio wala hamwezi kusikia.’”

184 Nikawazia, “Vema, kama Rais angekuja mjini badala ya uamsho, kila mtu angetoka aje. Loo, hakika, hayo ni mambo ya kilimwengu.”

185 Ndipo nikaanza kuwazia, “Vema, Mungu, vipi, kwa nini wewe huninii tu, vema, huji, umtume Yesu na tuyamalize? Kwa nini usininii tu—usiende ukayamalize yote, na uachane nalo?”

186 Ndipo nikaanza kuona kitu fulani kikisogea mbele yangu. Kilionekana kama kisulisuli kidogo kikizungukazunguka namna *hii*. Niliendelea kukiangalia. Nikaona ulimwengu ukizunguka-zunguka. Nikauangalia, na ambapo ulikuwa ukinyunyiza kitu fulani. Nikaangalia, na kilikuwa ni manyunyu mekundu, Damu nyekundu sana, toka upande mmoja hadi mwingine, kote ulimwenguni, kama tu kisulisuli kikizunguka, kama kimondo, na kilikuwa na kisulisuli namna *hii*. Ndipo nikakiangalia kisulisuli hiki. Na juu yake kidogo tu, nikamwona Yesu katika ono. Alikuwa akiangalia chini. Nami nikajiona nimesimama hapa duniani, nikifanya mambo nisiyopaswa kufanya. Na kila wakati nilipotenda dhambi, Mungu angaliniua, “Maana, siku utakayokula, siku hiyo utakufa.” Na utakatifu wa Mungu na haki Yake zinadai hilo, nawe ingekubidi ufe. Ndipo nikaangalia pale. Nikaendelea kusugua macho yangu. Nikasema, “Mimi si ninii. . . Sikulala usingizi. Mimi. . . Ni ono. Nina hakika hili ni ono.”

187 Niliendelea kuangalia, nilipokuwa nimesimama nyuma ya mlango. Ndipo nikaona dhambi zangu mwenyewe zikija. Na kila wakati zilipoanza kufika kwenye Kiti cha Enzi, Damu Yake ilifanya kama bamba la gari. Ilizishika, na ningeziona zikikitikisa, nayo Damu ingetiririka usoni Mwake. Nami nikamwona akiinua mikono Yake, na kusema, “Baba, msamehe, hajui atendalo.”

188 Nilijiona nikifanya jambo fulani lingine, likamtikisa tena, gonga. Ingeninii, Mungu angaliniua papo hapo, lakini Damu Yake ilikuwa ikinishika. Ilikuwa ikishikilia dhambi zangu. Nikawaza, “Ee Mungu, hivi nilifanya jambo hilo? Hakika haikuwa ni mimi.” Lakini ilikuwa ni mimi.

189 Ndipo nikaenda nikitembea namna *hii*, kana kwamba nilikuwa nikipitia kwenye kile chumba, ndipo nikatembea kwenda karibu Naye. Nikaona kitabu kimewekwa pale, kilikuwa kimeandikwa jina langu, na kila aina ya herufi nyeusi zimeandikwa humo. Nikasema, “Bwana, ninasikitika nilifanya jambo hili. Je! dhambi zangu zilikufanya ufanye hivyo? Je! nilimwaga Damu Yako kote ulimwenguni? Je! nili—

nilikufanyia jambo hili, Bwana? Ninasikitika sana kwamba nilifanya hivyo." Ndipo akanyosha mkono. Nikasema, "Je! utanisamehe? Sikutaka kufanya hivyo. Nitaninii . . . Wewe, kwa neema Yako, nitajaribu kuwa mvulana mzuri zaidi kama tu utanisaidia."

190 Aliinua mkono Wake akapigapiga ubavuni Mwake, akainua kidole Chake na akaandika "amesamehewa" kwenye kitabu changu; akakitupa nyuma Yake, Bahari ya Usahaulifu. Nililiangalia jambo hilo kidogo. Ndipo akasema, "Sasa, nimekusamehe, bali wewe unataka kumhukumu." Unaona? Kasema, "Umesamehewa, lakini vipi kuhusu yeye? Unataka kumlipua. Hukutaka aishi."

191 Nikawazia, "Ee Mungu, nisamehe. Sikutaka kuwazia namna hiyo. Sikutaka kufanya hivyo. Si—si—sikutaka kufanya hivyo."

192 "Umesamehewa. Unajisikia vizuri. Bali vipi kuhusu yeye? Anahitaji hilo, pia. Anahitaji hilo."

193 "Vema," nikawaza, "Mungu, nilijuaje ni nani Wewe umemwita, na ni nani hukumwita?" Kazi yangu ni kuzunguza na kila mtu.

194 Kwa hiyo, wakati hilo ono liliponiacha, nilimwendea. Nikasema, "U hali gani, bibi?" Na hao wanaume wawili walikuwa wamekwenda msalani. Nao . . . Alikuwa ameketi pale, akipiga kwikwi, mwajua, akicheka. Chupa ya wiski ikiwa hapo mezani, ama bia, ilikuwa ni kileo, kimewekwa pale, ambapo walikuwa wakinywa. Nilienda pale. Nikasema, "U hali gani?"

Naye akasema, "Mm, halo."

Ndipo nikasema, "Naweza kuketi?"

Akasema, "Loo, nina mtu."

Nikasema, "Sikumaanisha katika jinsi hiyo, dada."

Akaniangalia nilipomwita "dada." Akasema, "Unataka nini?"

Nikasema, "Naomba niketi kwa dakika moja."

Akasema, "Karibu." Nami nikaketi.

Nikamwambia jambo lililotukia. Akasema, "Jina lako ni nani?"

Nami nikasema, "Branham."

Akasema, "Wewe ndiye mtu uliye hapa chini kwenye uwanja huu wa michezo?"

Nikasema, "Naam, mama."

195 Akasema, "Nimekuwa nikitaka kuja kule chini." Akasema, "Bw. Branham, nililelewa katika familia ya Kikristo." Akasema, "Nina wasichana wawili vijana ambao ni Wakristo. Lakini mambo fulani, fulani yalinipata, naye akaendea njia mbaya, ama akaanza."

196 Nikasema, "Lakini, dada, sijali, ile Damu ingali inakuzunguka. Dunia hii imefunikwa na Damu." Kama isingalifunikwa, Mungu angetuua, kila mmoja. Yeye . . . Wakati Damu hiyo itakapoondolewa, tazamia hukumu. Lakini sasa, ukifa bila hiyo Damu, ukienda ng'ambo ya mahali hapo, basi hakuna kitu cha kuchukua mahali pako. Leo Damu inatenda kazi mahali pako. Nikasema, "Bibi, hakika, ile Damu ingali imekufunika. Mradi tu una pumzi mwilini mwako, ile Damu imekufunika. Lakini siku moja wakati hiyo pumzi itakapoondoka hapa, nafsi inatoka, utaivuka hiyo Damu, wala hakuna kitu ila hukumu. Wakati ukiwa na nafasi ya msamaha . . . " Ndipo nikamshika mkono.

197 Alikuwa akilia, kasema, "Bw. Branham, mimi ninakunywa pombe."

198 Nikasema, "Hilo halidhuru. Kitu Fulani kingine kimenionya nije nikakwambie." Nikasema, "Mungu, kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, alikuita, dada. Nawe unafanya makosa, na unalifanya tu kuwa baya zaidi."

199 Akasema, "Unafikiri Yeye anaweza kunikubali?"

200 Nikasema, "Kabisa, angekukubali."

201 Hapo akiwa amepiga magoti, tulipiga magoti katikati ya sakafu hiyo, na mkutano wa maombi ya mtindo wa kale. Huyo polisi akavua kofia yake na kupiga goti moja. Hapo tukawa na mkutano wa maombi, mahali hapo. Kwa nini? Mungu ni mkuu.

"Tukiweka kando matendo haya mafu, na tukaze mwendo tuufikilie utimilifu."

202 Hebu na tusogee tuingie kwenye milki ile ambamo mambo haya ya, "Mimi ni mfuasi wa kanisa; mimi ni mfuasi wa *lile*," hayo yote yamekwisha. Na tukaze mwendo tuufikilie ule utimilifu.

203 Rafiki yangu mwenye dhambi, kama wewe huna hiyo Damu leo, bila wokovu, bila neema, Damu ya Yesu Kristo inakushikilia. Unasema, "Vema, nimeliepuka wakati huu wote." Lakini siku moja unaenda mahali ambapo wakati huo hakuna kitu kitakachokusalia.

Hebu na tuombe sasa, wakati tunapoinamisha vichwa vyetu.

204 Je, kuna ninii, kungekuwako, na mtu mmoja hapa leo angetaka kusema, "Mungu unirehemu, ninatambua ya kwamba nimefanya makosa"? Huenda umejiunga na kanisa. Hilo ni sawa. Lakini kama hujapokea neema ya Kristo, unaweza kuinua mkono wako na kusema, "Niombee, mimi, Ndugu Branham"? Mungu akubariki, bwana. Mungu akubariki, mama. Naam. Usininii . . . Mungu akubariki, bwana, huko nyuma. Mungu akubariki, na wewe. Kule nyuma kabisa, naam, Mungu akubariki. Inua mkono wako. Naam. Inua tu mkono wako, na useme, "Mungu, unirehemu."

205 Unasema, “Mimi ni mfuasi wa kanisa, Ndugu Branham. Naam, ni—nimejaribu kuwa mtu mzuri. Lakini sijui, ninaonekana tu, inaonekana kana kwamba, siwezi kufanya hivyo.” Loo, maskini msafiri, maskini rafiki mdhaifu, wewe kweli ungali hujapata kuona hilo ono bado.

206 Unasema, “Ndugu Branham, nilipaaza sauti kwa nguvu. Nimenena kwa lugha. Nimefanya haya yote.” Huenda hilo ni kweli, pia. Hilo ni sawa, sina cha kusema dhidi ya hilo.

Lakini, rafiki yangu mpendwa, uliyepotea, lakini, kunena kwa lugha, au kutetemeka, au kupeana mikono, au kubatizwa, hayo, hayo ni sawa. Lakini, kumjua Yeye, ni kumjua Mtu. “Kumjua Yeye ni Uzima.”

207 Unasema, “Ninajua Biblia, vizuri sana.” Vema, kujua Biblia, si Uzima. “Kumjua Yeye,” kiwakilishi nafsi, “kumjua Yeye, Kristo,” kwamba unajua Yeye amekusamehe.

Ungeweza tu kuinua mikono yako, tena, mtu mwingine? Mungu akubariki, mama. Mungu akubariki wewe, bwana. Mungu akubariki wewe uliye hapa, ndugu. Mungu akubariki kule nyuma, ewe kijana mwanamume. Mungu akubariki hapa, dada. Mungu akubariki, huko nyuma kabisa, kule. Hiyo ni kweli. “Kumjua Yeye, ni Uzima.”

“Ndugu Branham, nikumbuke. Mimi sasa, papa hapa kitini pangu, nitamkubali Kristo.”

208 Sema, “Ingia moyoni mwangu, Bwana Yesu, na unipe ile amani, ule utamu.” Unaenda kanisani, unapiga muziki kwa nguvu uwezavyo, unacheza huku na huko, unakimbia kwenye marefu ya kanisa, unaenda nyumbani ukiwa mchovu, na unagombana na kuzozana, huyo si Kristo. Unaenda kanisani, unaketi na kusikiliza mahubiri mafupi kuhusu vile daraja litakavyopakwa rangi, ama kitu fulani, kitu kingine kama hicho, kamwe husikii Neno. Neno huleta Uzima. Ni Mbegu. Hivi hutaki amani?

209 Je! unaona wasiwasi juu ya kufa? Ungeweza kuwa na mshtuko wa moyo leo, je! hilo linakusumbua? Ama ungefurahi, kusema, “Ninaenda kuwa pamoja na Bwana Yesu kwenye mwisho wa njia hii”? Je! unamjua? Kama humjui, inua tu mkono wako. Tutawaombea. Naam, ndugu, wewe, pia.

210 Vema, moyoni mwako sasa.

> Hivi nilivyo tu, bila hata kisingizio kimoja,
> Ila kwamba Damu yako ilimwagwa (kwa ajili ya nani?) kwa ajili yangu,
> Kwa maana ninaahidi, nitaamini,
> Ee Mwana-Kondoo, Ee Mwana-Kondoo wa Mungu, naja. Naja, kwa upole, kwa rehema.
>
> Hivi . . .

Njoo tu Kwake, kwa imani. Amini ya kwamba Yeye anasimama papo hapo karibu nawe. Anasimama.

> . . . -ngojea
> Kuitua mzigo nafsi yangu (mangapi sasa?)
> moja ya hayo . . . (hasira, chuki),
> Kwake Yeye ambaye Damu Yake inaweza
> kusafisha kila waa,
> Ee Mwana-Kondoo . . .

211 "Kwa imani nitakwenda msalabani, asubuhi ya leo. Nitashusha mizigo yangu. Ninakuja." Mungu akubariki huko nyuma. Hilo ni zuri. [Ndugu Branham anaanza kuvumisha *Nitwae Hivi Nilivyo*—Mh.] Usiwe mtu asiyejali sasa. Kwa furaha, uchangamfu, tembea uende moja kwa moja msalabani.

212 Katika Agano la Kale, walileta mwana-kondoo. Walijua walikuwa wamefanya dhambi, walijua jambo hilo kwa zile amri. Unajua jambo hilo sasa, kwa kuwa Mungu amenena kwenye moyo wako. Waliangalia zile amri, "Usizini. Usifanye *hivi na vile*." Nao wakamchukua mwana-kondoo, wakaenda na wakaweka mikono yao juu ya mwana-kondoo, kuhani akamchinja. Maskini jamaa huyo alikuwa akipiga mateke, na kutokwa na damu, na kulia, na kufa. Mikono yake yote ilikuwa imefunikwa na damu. Huyo mwana-kondoo alikufa mahali pake, bali aliondoka hapo akiwa na tamaa ile ile ya kufanya jambo hilo tena.

213 Lakini mahali hapa, tunakuja kwa imani, kwa neema. Mungu alituita. Tunaweka mikono yetu juu ya kichwa cha Mwana-Kondoo wa Mungu. Tunaisikia hiyo nyundo inayozungushwa. Tunasikia hiyo Sauti, "Ninaona kiu; nipe maji ninywe. Baba, usiwahesabie dhambi hii; hawajui watendalo." Unaona? Kwa imani, tunahisi mauti Yake pale badala yetu. Ndani kabisa moyoni mwetu inakuja amani kuu iliyotulia, wakati Sauti fulani inaposema, "Umesamehewa sasa. Nenda na usifanye dhambi tena." Vipi, kwa neema, basi, tunaondoka pasipo na tamaa ile ile, bali hamu ya kutotenda dhambi tena ama kufanya lolote baya. Amani inayopita ufahamu wote, imeingia moyoni mwetu.

Naomba mwipokee sasa tunapoomba, kila mmoja, pamoja.

214 Baba wa Mbinguni, wanakuja kwa imani, kwa njia ya neema. Kuna kama dazani moja ya mikono iliyoinuliwa. Ni matunda ya Ujumbe huu. Wanakuja Kwako. Wanaamini. Ninawaamini, pia, Bwana. Ninaamini ya kwamba, hakika, Roho Mtakatifu alinena nao. Na kwa imani wanapanda moja kwa moja kwenye ngazi ya Yakobo sasa, moja kwa moja mpaka chini ya msalaba, hapo wanaweka dhambi zao zote chini, na kusema, "Bwana, zimenilemea mno. Siwezi tu kuzivumilia tena. Na nakusihi uondoe mzigo wangu wa dhambi, na utoe tamaa ya kufanya jambo hilo moyoni mwangu? Na nijalie, kwa imani,

leo hii, nikupokee Wewe kama Mwokozi wangu binafsi. Na tangu sasa, nitakufuata kila maili ya njia, hata mwisho wa safari yangu. Nimetupia jicho kile inachomaanisha 'kukaza mwendo kuufikilia utimilifu,' si kwenda kanisani, na mashina ya matendo mafu kama mabatizo na kadhalika. Lakini ninataka kuendelea, mpaka isiwe tena ni mimi, na Kristo anaweza kuishi ndani yangu."

215 Ee Yesu, lijalie jambo hili kwa kila nafsi yenye kutubu, asubuhi ya leo. Kila mtu aliyeinua mikono yao atapokea Uzima wa Milele kwa sababu Wewe uliuahidi. Walikubali mbele za watu. Wanainua mikono yao. Walivunja kanuni zote za uvutano. Waliifanya sayansi wajionee aibu, maana sayansi inasema, "Mikono yako haina budi kuning'inia chini." Chochote kingeweza kuthibitisha jambo hilo katika sayansi, ya kwamba haina budi kushikiliwa chini na dunia hii, kwa maana uvutano unaishikilia chini. Lakini kulikuwa na roho fulani ndani yao iliyofanya uamuzi, nao wakaasi kanuni za uvutano na kuinua mikono yao. Uliliona hilo, Bwana. Uliandika jina lao katika Kitabu. "Wamesamehewa." Kitabu hicho cha kale kimerudishwa kwenye Bahari ya Usahaulifu sasa, kisije kikakumbukwa tena. Jalia wasonge mbele leo, kama Wakristo wanaopendana, wenye upendo, wapate kukutumikia. Na labda wako wengi ambao hawakuinua mkono wao, wajalie pia.

216 Jalia watakatifu watembee tu karibu kidogo zaidi, Bwana, kwa maana tumekaribia Nyumbani kwa siku moja zaidi kuliko tulivyokuwa jana. Uwe pamoja nasi, Bwana, kwa maana tunaomba katika Jina la Kristo na kwa ajili ya utukufu Wake. Amina.

*Kitabu Cha Waebrania*

Jumbe hizi kumi na moja za Ndugu William Marrion Branham zilizohubiriwa hapo awali katika Kiingereza kutoka tarehe 21 Agosti mpaka tarehe 22 Septemba, 1957, katika Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, U.S.A., zimetolewa kwenye kanda za sumaku zilizorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice of God Recordings. Ilichapishwa tena katika mwaka wa 2013.

SWAHILI

©2009 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

Voice Of God Recordings
P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.
www.branham.org